Alhamisi Novemba 16, 2023 • Tanzania 1000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581496
www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



ALHAMISI NOVEMBA 16, 2023

ama

AFYA NA MAZINGIRA

Ukurasa 12
Mageuzi; kliniki tembezi kuwafuata waliko wenye malaria na Ukimwi

Ukurasa 13
BINGWA AFUNGUKA UZAZI MPANGO; Orodha mambo muhimu maishani, watumiaji wajibebesha mengi

Ukurasa 14
Dk. Bingwa: Tunayoishi nayo kifamilia, ni janga masikioni mwa watoto

MAZINGIRA

Karipio la Rais uharibifu wa Mto Ruvu, Pwani lilivyobeba jukumu

Na Mwandishi Wetu

• Anafuatilia kwa hatua, mama atue ndoo...
• Kisa na mkasa; mifugo, kilimo umwagiliaji

SURA zote za uongozi wa nchi, hazifichi ishara namna mkuu wa nchi alivyojielekeza katika sekta ya maji, kuna wakati anakuwa nayo jirani mithili ya waziri mwenye dhamana.

Hiyo inakuja, huku kinamama wakiwamo taasisi ya TGNP, mwanaharakati mkubwa wa jinsia nchini katika yale wanayoyahesabu mafanikio ya Rais Dk. Samia katika miaka yake miwili ya uongozi, ni pale anakuwa mbia wao wa kampeni 'kumtua ndoo mama'.

Kimsingi, ni hatua inayohimiza upatikanaji huduma ya maji kitaifa kuondoa shida hiyo katika umma nchini, kupata maji katika umbali mdogo. Rais Dk. Samia, hakuficha hisia zake kwa waziri mteule, Jumaa Awesu akimtamkia msimamo wake "ukinizingua, nitakuzingua." Kimsingi, ni onyo zito hata akashuhudiwa mbunge huyo wa mkoani Tanga, akiwajibikia maji kweli kweli, kukidhi mahitaji ya aliyemteua.

Baada ya wastani miaka miwili, Dk. Samia akarejesha kuridhika na mheshimiwa Awesu anavyotumika, akimpa kongole na timu yake ya kazi, alipowatamkia:

"Zamani huko nilikuwa na ugomvi na watu wa maji. Kwa sasa, watu wa maji ni marafiki zangu kweli kweli! Wizara imebadilika. Taasisi zilizoko chini ya wizara zimebadilika, kazi inafanywa kweli kweli na naomba mwen-

Hali halisi ya mifugo, inayotajwa kuathiri upatikanaji wa maji katika Mto Ruvu, hata Rais akakemea mwenendo huo. PICHA: MTANDAO

Ni ishara inayozaliwa na dhana 'ukiona vyaelea vimeundwa.' Daima Rais Dk. Samia, mbali na kueleza utekelezaji, ni mfuatiliaji wa karibu wa miradi ya maji, kukagua na hata uzinduzi wa miradi, hata kugawana majukumu na makamu wake, Dk. Philip Mpango.

Mfano hai ni kilichoripotiwa na gazeti hili wiki kadhaa zilizopita

kutoka Ziwa Victoria, katika mikoa ya Simiyu iliyofanywa mwezi Februari na Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango na kisha mkoani Singida, siku kadhaa zilizopita, ikafanywa na Rais Dk. Samia.

Katika shughuli kama hiyo kwenye Mradi wa Maji Bonde la Mto Ruvu, Rais Dk. Samia, akawa mkali baada ya kupata taarifa ya ku-

mtiririko wa maji katika mto huo.

Hapo inajumuisha unyweshaji mifugo, pia baadhi ya wakulima wanaotumia mifumo ya Mto Ruvu kumwagilia, akaagiza mamlaka ya mkoa kuchukua hatua kudhibiti na kufanyika tathmini mpya.

MKOANI PWANI

Baada ya agizo, uongozi wa

kutekeleza maagizo ya Rais Dk. Samia, kusafisha bonde la Mto Ruvu ili kuwezesha upatikanaji maji kwa matumizi ya binadamu.

Mwezi kama huu, Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge akatoa taarifa kwa Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango, kuhusu hatua zinazochukuliwa na mkoa kutekeleza maelekezo ya Rais Dk. Samia.

Msingi wake, lengo likawa kuondoa upungufu wa maji kwenye bonde hilo unaosababishwa na shughuli za kibinadamu, mkuu wa mkoa akiwa na ufafanuzi kazi hiyo ilifanyika kwa kutumia helikopta: Anataja kwamba wamebaini kuwapo mifugo mingi, maji kuchepushwa, lakini kwa wakati huo baadhi ya maeneo yakarejeshwa chukuliwa kudhibiti hali hiyo.

"Tuliamua kuwaelekeza wale wote wanaotumia maji, kuendesha kilimo cha umwagiliaji kwa njia halali (wenye vibali), wasitishe kwa muda, wasio na vibali pamoja na wenye mifugo kuacha mara moja na wameacha.

"Lakini, operesheni zinaendelea na kukamata watumiaji wasio na vibali na watakaokaidi maagizo na maelekezo haya."

Kunenge akabainisha kuwa, ofisi yake ilitumia utaratibu bora wa kufanya mikutano na wadau, iliyosaidia kubaini na kudhibiti uchepushaji maji na kuzuia ukataji miti, ili kutunza vyanzo vya maji.

UKURASA 11

**MWINYI** ataka sera, sheria wezeshi haki za kiuchumi



UKURASA 3

**TMA** yatangaza mvua kubwa hadi Jumamosi, yataka kuwapo tahadhari

UKURASA 4

**MVUTANO** waibuka hospitali kuvamiwa Ukanda wa Gaza

UKURASA 19

# Rufani kesi mama nyama swala yaiva

## MAWAKILI

wafungua kesi kupinga hukumu, wasubiri Jaji, tarehe... *Endelea Ukurasa wa 2*







Mwenyekiti wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) Mkoa wa Iringa, Moses Ambindwile (katikati) na Mwenyekiti wa Dawati la Msaada wa Kisheria TLS Mkoa, Mchungaji Joshua Chusi (kulia), wakiwa na Mwanasheria wa UWT, Abdul Marijani, wakitoka katika Mahakama Kuu Kanda ya Iringa jana, kuthibitisha usajili wa rufani ya Maria Ngoda. **Picha kulia**, Ngoda akiwa chini ya ulinzi wa askari polisi baada ya kuhukumiwa kifungo miaka 22. **PICHA: GODWIN/ MTANDAO**

# Makonda awapasha wenye ndoto kuwania urais 2025



UKURASA 2



Sehemu ya mwonekano wa mabaki ya baadhi ya zaidi ya vyumba 150 'madanguro' vilivyokuwa vikitumika kwa biashara ya ukahaba katika eneo la Mwananyamala, Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam, baada ya kubomolewa na serikali hivi karibuni. **PICHA: HALFANI CHUSI**

UKURASA WA 22

## UNITED YAJIANDAA KUMKOSA ONANA



MANCHESTER United wamejipanga kumkosa, André Onana wakati wa michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2023), Januari...

## Chanjo ya lazima kwa mifugo yaja

UKURASA 3

**MICHEZO** SIMBA SC KUMPA RUNGU KOCHA KUBORESHA KIKOSI UK. 24

**KATUNI** UK. 6



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akikagua ujenzi wa zahanati ya Kijiji cha Namilema iliyojengwa kwa nguvu za wananchi, wakati akiwa katika ziara ya kukagua miradi ya maendeleo Wilaya ya Ruangwa, mkoani Lindi jana. **PICHA: OWM**

# Rufani kesi mama nyama swala yaiva

**Na Francis Godwin, IRINGA**

JOPO la mawakili 10 wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) na Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), limekamilisha usajili wa rufani ya mjane Maria Ngoda, aliyefungwa jela miaka 22 kwa kukutwa na vipande 12 vya nyama ya swala kinyume cha sheria.

Akizungumza jana na Nipashe nje ya viwanja vya Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Iringa, Wakili wa TLS, Moses Ambindwile, alisema usajili wa kesi hiyo ulikamilika jana saa 7:00 mchana.

Alisema kimsingi usajili wa awali ulifanyika Novemba 13 majira ya jioni lakini kutokana na changamoto za mfumo wa kielektroniki uitwao 'Electronic Case Management System (eCMS), walikwama kupata namba ya usajili wa kesi hiyo.

Kutokana na mazingira hayo, alisema walilazimika kufanya mchakato mpya wa usajili wa kesi hiyo na sasa wamepata namba.

"Siku ya Novemba 14, 2023 majira ya mchana, rufani ya Maria Ngoda ilifanikiwa kuingizwa katika mfumo mpya wa kusajili mashauri kwa njia ya kielektroniki uitwao Electronic Case Management System (eCMS). Hatua inayofuatia ni upande wa mahakama kuisajili rufani hiyo na kutoa 'summons' (hati ya wito) kwa ajili ya hatua ya usikilizwaji," alisema Wakili Ambindwile.

Wakili Ambindwile ambaye alikuwa ameongoza na Wakili Mchungaji Joshua Chusi ambaye ni mwanasheria wa UWT na Abdul Marijani, alisema namba ya usajili (Admission) ni 84101 /2023 Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Iringa.

Mbali ya Wakili Mchungaji Chusi ambaye ni Mwenyekiti wa Dawati la Msaada wa Kisheria katika Ofisi za TLS Iringa, aliwataja mawakili wengine walioko katika jopo hilo kuwa ni Dk. Rwezaula Kaijage, Frank Ngafumika, Barnabas Nyalusi, Jane Massey, Samson Rutebuka, Innocent Kibadu, Cosmas Kishamawe na Jali Mongo.

Alisema yeye atakuwa kiongozi wa jopo la mawakili hao huku mwanasheria wa UWT atawasaidia kufanya utafiti.

Wakili Ambindwile alitoa wito kwa mawakili wengine wanaohitaji kuongeza nguvu zaidi kwenye rufani kuwa wanaruhusiwa kujitokeza.

Kwa mujibu wa Ambindwile, baada ya kusajili kesi hiyo, wanasubiri mahakama ipange jaji wa kusikiliza na kwamba wana uhakika ndani ya siku 45 watakuwa wamepata jaji kama utaratibu unavyobainisha.

Naibu Msajili wa Mahakama Kuu Kanda ya Iringa, Malewo Maximillian, alithibitisha kusajiliwa kwa kesi hiyo na kwamba hatua inayofuata ni kupanga jaji wa kusikiliza.

Hukumu dhidi ya Ngoda ilitolewa Novemba 3, mwaka huu na Hakimu Mkazi Mkuu Said Mkasiwa wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Iringa baada ya kusikiliza ushahidi wa pande zote na kujiridhisha.

Mwanamke huyo mwenye watoto wanne, alikutwa na ndoo ikiwa na nyama ya swala yenye thamani ya Sh. 900,000, kosa ambalo ni kinyume cha Sheria ya Wanyamapori.

Akitoa hukumu kwa mjane huyo mkazi wa Zizi la Ng'ombe, Manispaa ya Iringa, Hakimu Mkasiwa alisema kosa hilo ni kinyume na kifungu cha 86 (1) (2) (c) cha Sheria ya Wanyamapori Na. 5 ya Mwaka 2009 kama ilivyofanyiwa marekebisho na kifungu cha 59 (a) (b) cha Mabadiliko ya Sheria ya Mwaka 2016.

Wakati akijitetea bila usaidizi wa wakili, mjane huyo alikiri kukutwa na ndoo yenye nyama hiyo, huku akidai alikabidhiwa na mtu aliyejitambulisha kwa jina moja la Fute bila kujua ni ya mnyama gani.

Alidai kuwa alilazimishwa abebe ndoo hiyo na kufikishwa kituoni kisha kufunguliwa kesi ya kukutwa na nyara za serikali sambamba na kosa la uhujumu uchumi.

Tangu kutolewa kwa hukumu hiyo, kumekuwa na mjadala mkubwa kwenye mitandao ya kijamii, huku wengi wakishangazwa na kutaka msaada zaidi wa kisheria kwa mwanamke huyo.

# Makonda awapasha wenye ndoto urais 2025

**Na Beatrice Shayo, BUTIAMA**

KATIBU wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Paul Makonda, amesema bado kuna mafisadi nchini wenye ndoto ya urais mwaka 2025 na ziara yake imewavuruga.

Aliyasema hayo jana baada ya kuweka shada la maua katika kaburi la Hayati Mwalimu Julius Nyerere, nyumbani kwake wilayani Butiama, mkoani Mara.

"Ombi langu moja ninaloliomba wazee wangu, msiache kuniombea, mafisadi kwenye hii nchi bado hawajaisha, watu wanaopenda kudhulumu watu hawajaisha, watu wasiokuwa na sifa ya uongozi wanaotaka uongozi hawajaisha, kwa hiyo wakituona watu tunasimamia haki hawapendi, wanatafuta kila namna ya kuchonganisha viongozi na mpasuko kwao ni mafanikio," alisema Makonda.

Amemshukuru Mwenyekiti wa chama hicho, Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwa makini, shupavu, mahiri, msikivu, mtulivu na anayepima mambo kwa upana wake na kwamba ziara yake imewavuruga wenye ndoto za urais.

"Hii ziara tuliyofanya Kanda ya Ziwa imewavuruga kweli... hasa wenye ndoto za urais sasa wao walifikiri watamchezea mwenyekiti wetu wa chama mwaka 2025 wakiyumbishe wapate nafasi, nimewaambia lahasha na mmenipa hii fimbo nitawachapa," alionya.

Kadhalika, alimshukuru Mungu kufika katika familia ya Baba wa Taifa na kupewa upendeleo wa kulala kwenye makazi yake na kupata usingizi mzuri ambao umemwepusha ndoto za ajabu na kutoa mfano wa maeneo mengine ambayo akilala anapambana, anaamka amechoka.

"Nimekuja kuwaeleza viongozi wangu kwamba tupo pamoja katika kuenzi na kutambua na kuheshimu kazi ya Baba wa Taifa katika taifa hili na maneno yangu sio kwamba tupo pamoja kwa sababu ya maneno ya kisiasa, nina maanisha ndio maana nilivyofika kwenye kaburi la Hayati John Magufuli, nilieleza mimi sio mtu wa lugha mbili na hapa ninasema Mwalimu nitamuenzi, sikuwapo wakati anaongoza katika ufahamu huu nilionao na sikushiriki harakati zake, lakini alama zake njema, sifa zake, uadilifu na utumishi wake kwa taifa bado unasomeka katika kurasa za Tanzania na hata nje ya nchi anajulikana, mimi ni nani niache kumuenzi?" Alihoji.

Alisema, ameijulisha familia ya Baba wa Taifa kuwa wapo viongozi wanamuenzi Mwalimu Nyerere kwenye majukwaa, lakini matendo yao hayafanani na Mwalimu na kusisitiza hataki kuwa kama wao, anataka kuwa tofauti kwa sababu hofu ya Mungu ni msingi wa maisha yake.

Alisema waliyoyazungumza katika kikao cha ndani na familia, ana imani wataenda kuyafanyia kazi kwa kadri ya mapenzi ya Mungu na kuyatekeleza.

"Naomba nitoe rai, tunapoiona familia ya Mwalimu au viongozi wetu, Abeid Amani Karume, Benjamin Mkapa au John Magufuli, hizi familia kuna mambo waliyakosa kwa sababu ya utumishi wa taifa, walikosa muda wa kukaa na ndugu zao kuna muda walijinyima wakiona wakifanya wataonekana wanajipendelea, walifanya kwa ajili yetu tunapokutana nao tuwaheshimu kwa sababu kwa namna moja wameshiriki kujenga taifa, wazazi wao kutowatumikia wao wakatutumikia Watanzania wote bila kubagua dini, kabila na elimu nakuahidi Mwalimu huko alipo atafurahi," alisema Makonda.

Akizungumzia Katiba ya mwaka 1977, alisema waasisi wameweka misingi thabiti ya chama kiwe cha kutetea wanyonge, sauti ya kila Mtanzania, chama kisichobagua na kusimamia haki.

Alisema licha ya fimbo aliyopewa kama alama, Mwalimu yupo kwenye mioyo ya Watanzania atahakikisha heshima yake, kazi zake nzuri alizozifanya zinaendelea kuwa kumbukumbu kwa nchi na vizazi vijavyo.

Msemaji wa familia ya Mwalimu Nyerere, Chifu Japheth Wazagi, alisema familia inamshukuru Rais Samia na wasaidizi wake kwa kuwa hajawaacha, yupo karibu nao katika shida na raha.

"Siku zote tunaendelea kukiombea Chama Cha Mapinduzi na serikali iliyopo madarakani, tunatambua misingi ya mwasisi wake ni huyu Baba yetu ambaye ni Baba wa Taifa, siku zote tunaomba mema kwa ajili yetu na kwa chama na imani Watanzania wana imani na Chama kwa sababu ya misingi imara iliyowekwa," alisema Wazagi.

Ameomba viongozi wote kuendelea kujenga misingi hiyo na kuisimamia kwa kuwa ni chama ambacho alikianzisha Baba wa Taifa kinachoisimamia serikali katika misingi ambayo iliasisiwa.

Alisema wanaliombea taifa na wanapoingia kwenye uchaguzi mwakani wa serikali za mitaa wapate ridhaa katika ngazi za serikali za mitaa na wapate ushindi katika Uchaguzi Mkuu unaotarajia kufanyika mwaka 2025 waongoze nchi katika misingi ya amani na haki.

"Watu wana imani kwa sababu haki inatendeka tunaendelea kukiombea chama chetu na serikali iliyopo madarakani,"

# Mwinyi ataka sera, sheria wezeshi haki za kiuchumi

**Na Romana Mallya**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema mawaziri wanapaswa kutunga sera na sheria wezeshi zitakazosaidia wanawake na vijana kutengeneza ajira zenye staha katika sekta rasmi na isiyo rasmi ili kufikia haki ya kiuchumi.

Amesema lengo lisiwe kutengeneza ajira pekee, bali kuhakikisha kuwa, wanaweka sheria inayolenga kuondoa ujinsia.

Mwinyi aliyasema hayo jana Dar es Salaam wakati akifungua mkutano wa mawaziri wa Afrika kuhusu uwekezaji kwa maendeleo ya usawa wa jinsia huku akisisitiza kuwa Tanzania itaendelea kujikita katika usawa wa kijinsia.

"Leo tuna nchi 21 katika bara zima zinazowakilishwa na mawaziri wa wizara za fedha pamoja na za wanawake na masuala ya jinsia waliokusanyika hapa ili kujadili umuhimu wa ahadi za kikanda kuhusu ufadhili wa usawa wa jinsia.

"Mkutano huu wa kikanda unaakisi dhamira ya serikali za Afrika kufanya kazi pamoja na kutoa ushirikiano thabiti miongoni mwa viongozi wa Afrika kama 'kanda moja na jumuiya moja' inayojitolea kufikia malengo ya Agenda 2063 na Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030.

Alisema ni muhimu viongozi kuthibitisha kujitolea katika kufanya kila juhudi kutafsiri hatua muhimu za muungano wa haki ya kiuchumi ya kizazi na haki ya kiuchumi, ili kuwa mfano wa vizazi vijavyo Afrika.

Mkutano huo, alisema unatarajiwa kufafanua upya kasi ya kutimiza ahadi za usawa ifikapo mwaka 2026, hivyo wanajukumu muhimu la kutekeleza.

Alisema, Tanzania imejitolea kukabiliana na ukosefu wa usawa wa kijinsia katika nyanja zote za maisha ya wanawake.

"Kipengele cha jinsia kimeunganishwa kikamilifu katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26), na Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2025, zote zinasisitiza kujitolea kukuza usawa wa kijinsia katika muktadha wa kijamii, kiuchumi na kisiasa," alisema.

Pia alisema, serikali imepitisha na kutekeleza mageuzi kadhaa ya kisera yakiwamo maboresho ya hivi karibuni ya Sera ya Maendeleo ya Jinsia Tanzania ambayo yameweka mfumo wa kuimarisha usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake katika masuala ya upatikanaji wa elimu, afya, ajira na ardhi.

"Ubaguzi mahali pa kazi katika kuajiri, kupandisha vyeo, malipo, mafunzo na kupata nafasi za kufanya uamuzi. Zaidi ya hayo, tunahitaji kuunda mfumo wa mageuzi ya sheria na utekelezaji wa sera kuhusu maisha ya kazi yenye usawa wa kijinsia," alisema.

Pia alisema, wanahitaji kuondoa sera zote za ubaguzi wa kijinsia, kupitisha na kutekeleza sheria na sera na kuweka mikakati na uwekezaji unaowezesha kupatikana kwa haki za wanawake na wasichana.

Alisema ili kufanikisha hilo, lazima waimarishe uingiliaji kati wa kukuza mabadiliko ya kitamaduni, ili kubadilisha kanuni za kijamii za kibaguzi na majukwaa ya usaidizi yanayowakilisha vikundi vya wanawake.

"Ni lazima pia tufanye kazi ili kuwapa wanawake fursa ya kufikia na kutumia rasilimali za uzalishaji, ikijumuisha mtaji wa bei nafuu, huduma za kifedha, bidhaa za kidijitali, na kukuza ushirikishwaji wa kifedha wa wanawake kupitia mbinu bunifu," alisema.

Katika mkutano huo, Rais Mwinyi alieleza mafanikio mbalimbali ambayo Tanzania imeyafikia katika kuongeza upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wanawake.

Alisema pengo la jinsia katika ushirikishwaji wa fedha limepungua kutoka asilimia 10 mwaka 2017 hadi asilimia nne mwaka 2023 na kumekuwa na ongezeko la asilimia ya wanawake wanaotumia huduma za kibenki kutoka asilimia 66 mwaka 2017 hadi asilimia 80 mwaka 2023.

Alisema utumiaji wa kanuni za upangaji bajeti unaozingatia jinsia ili kufuatilia matokeo ya kijinsia na kutathmini athari za sera za fedha zinazozingatia jinsia, kunaweza kuchangia matokeo ya maendeleo endelevu ambayo wanatafuta.

Rais Mwinyi alisema Rais Samia Suluhu Hassan, amekuwa kinara kuhakikisha kwamba, wanawake wanafanya vizuri katika suala la uchumi.

Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema usawa wa kijinsia unasaidia kukuza uchumi wanawake na kwamba, Rais Samia amekuwa nguzo ya mafanikio kwa wanawake wengine hasa katika suala la usawa wa kijinsia.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, alisema mkutano huo ni wa kihistoria na umechangiwa na juhudi za Rais Samia kufanya uamuzi thabiti wa kuwekeza katika kuendeleza wanawake na maendeleo ya masuala ya jinsia.

Katika mkutano huo ambao warishiriki kujadili namna bora ya kushughulikia athari za mapungufu ya kijinsia katika uchumi wa jumla ambapo, Mwakilishi wa UN Women, alibainisha kuwa usawa wa kijinsia unahusu maendeleo ya taifa.



Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Halima Dendego (katikati), akizungumza wakati akitangaza siku ya kuanza kwa operesheni endelevu ya safisha mji ya kuwaondoa wafanyabiashara holela, mjini Iringa jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Chanjo ya lazima kwa mifugo yaja

**Na Gwamaka Alipipi**

SERIKALI inatarajia kuanzisha utaratibu wa kutoa chanjo ya lazima kwa mifugo kila baada ya miezi mitatu lengo likiwa kuzuia magonjwa kwa mifugo, binadamu na kuipa thamani nyama ya Tanzania katika masoko ya kimataifa.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alisema hayo jana Ikulu, jijini Dar es Salaam, wakati wa mkutano na waandishi wa habari uliolenga kutoa mrejesho wa ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan aliyoifanya Morocco na Saudi Arabia hivi karibuni.

Ulega alisema hivi sasa kuna tatizo kubwa la mifugo nchini kushambuliwa na magonjwa yanayosababisha athari mbalimbali vikiwamo vifo, magonjwa kwa binadamu pindi anapokula nyama yenye vimelea vya wadudu na nyama kutokukidhi ubora katika masoko ya kimataifa.

Alisema kutokana na hali hiyo, wizara inatarajia kuanzisha kampeni ya kuchanja mifugo kwa lazima kwa utaratibu maalum na kampeni hiyo itazinduliwa na Rais Samia. Mbali na kampeni hiyo, alisema Rais Samia pia atazindua kiwanda kitakachotengeneza chanjo hizo.

"Utawekwa utaratibu maalum wa kuchanja, kama ni kila baada ya miezi mitatu, kwamba kila mfugaji atalazimika kuchanja mifugo yake. Tunataka tuuze kwa wingi nyama katika soko la kimataifa, pamoja na kuzuia magonjwa yatokanayo na kula nyama yenye virusi," alisema Ulega.

Ulega alisema mwaka 2021 Tanzania iliuza nyama tani 1,700 katika soko la dunia na hadi sasa tani 14,000 zimeshauzwa kiasi ambacho ni kidogo.

Alisema hadi Juni, mwaka huu Saudi Arabia ilinunua tani 1,400 za nyama kutoka Tanzania huku mahitaji yao yakiwa ni tani 21,000.

"Bado tunafuga kizamani, tunafuga kimila. Tunatakiwa tufuge kibiashara, tunatakiwa tupeleke mifugo sokoni. Ni kweli mifugo ni utajiri lakini ni lazima ifike sokoni," alisema Ulega.

Mkurugenzi wa Mashariki ya Kati kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Abdallah Kilima, aliwasihi Watanzania wanaokwenda kufanya kazi katika nchi za Mashariki ya Kati wafuate utaratibu ili wawe salama.

Alisema nchi za Mashariki ya Kati zinategemea nguvu kazi kutoka kwa wageni wanaofika kufanya kazi.

Balozi Kilima alitolea mfano akisema Oman ina idadi ya watu milioni tano lakini watu milioni 2.4 ni wageni. Kati ya wageni hao, kutoka India ni 800,000 na Wapakistan ni 300,000. Pia alisema Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) asilimia 60 ya wakazi wake ni wageni.

Alisema asilimia 92 ya taarifa kwamba wageni wanateswa katika nchi za Mashariki ya Kati si kweli, akitolea mfano kwamba kuna Watanzania 25,000 Oman kati yao 17,000 wanafanya kazi za ndani.

"Wafanyakazi wa ndani Oman kima cha chini wanalipwa Dola za Marekani 300 kwa mwezi. Wako Watanzania wanaohudumia familia zao huku Tanzania kwa kazi wanazofanya Oman. Ukifuata utaratibu hutapata matatizo," alisema.

Mkurugenzi wa Uhamasishaji Uwekezaji kutoka Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), John Mathew, alisema kuanzia Julai hadi Septemba, mwaka huu, TIC imeandikisha miradi 137 na kutengeneza ajira 86,900.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
16.11.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Jumamosi tarehe 18-11-2023 hadi 20-11-2023 kampuni ya Mainline Carriers Ltd itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka Dar-Es-Salaam Port kuelekea Kilombero kupitia Mikumi, gari hizo zina namba za usajili: **T 289 EDD /T 879 EAU T 204 DYJ / T 881 EAU T 203 DYJ /T 568 EAZ**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita 20.00** |
| **Upana** | - | **mita 4.20** |
| **Kimo** | - | **mita 5.40** |

2. Njia itakayotumika: Dar-Es-Salaam, hadi Kilombero kupitia Mikumi, gari zitasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

## Washauri kusitisha matumizi ya zebaki matibabu ya meno

**Na Christina Mwakangale**

SHIRIKA la Maendeleo na Mazingira na Kudhibiti Kemikali (AGENDA), kwa kushirikiana na Sauti ya Walaji Tanzania na Utafiti (TCAR), limeishauri serikali na madaktari wa afya ya kinywa na meno, kusitisha matumizi ya zebaki kutokana na athari za kiafya na kimazingira.

Miongoni mwa athari zilizotajwa ni uoni hafifu, usikivu, viungo kupooza, ukosefu usingizi, ongezeko la hasira pamoja na kuathiri mfumo wa uzazi, ikiwamo mbegu za kiume.

Ofisa Programu Mwandamizi wa AGENDA, Dorah Swai, aliyasema hayo jana kuhusu Wiki ya Afrika ya Kupinga Matumizi ya Dawa Yenye Zebaki ya Kuziba Meno Yaliyotoboka, iliyoanza Novemba 13 na inataraja kufikia tamati keshokutwa.

"Madhara ya zebaki pia ni wakati wa kuzaliwa mtoto, mimba kutoka. Lengo kuu la mwaka huu ni kuitaka serikali na madaktari wa afya ya kinywa na meno, wasitishe kutumia dawa yenye zebaki ya kuziba meno yaliyotoboka kwa kutumia amalgam.

"Tunatarajia iwe hivyo pia kwa makundi mengine siku zijazo. Huu ni mwaka wa 10 tangu tuanze kushiriki maadhimisho haya kuanzia yalipozinduliwa mwaka 2014," alisema Swai.

Alisema wito huo unaendana na matakwa ya Mkataba wa Minamata uliopitishwa mwaka 2013 na nchi 140, Tanzania ikiwamo na baada ya kupitishwa, Tanzania kuuridhia Oktoba 5, 2020.

"Marekebisho kadhaa yamefanyika kwa Mkataba huu likiwamo marekebisho kwa watoto linalozitaka nchi wanachama kutotumia 'Dental Amalgam' kwa kuzibia meno ya watoto, wajawazito na wanaonyonyesha," alisema.

Katibu Mtendaji wa AGENDA, Haji Rehani, alisema amalgam ina zebaki kwa asilimia 50 na inadhuru wanadamu na mazingira huku akisema hatua hiyo ni kutoa wito kwa jamii na utekelezaji wa Mkataba wa Minamata ambao umepitishwa na kuridhiwa na Tanzania.

"Tunaitaka serikali kukuza kasi ya usambazaji wa taarifa kwa madaktari, sekta ya umma na binafsi na kwa wananchi, ambao ndio walaji wa huduma hizi.

"Wananchi wana haki ya kuchagua dawa ya kuzibia jino ila wanaweza kufanya hivyo kama watakuwa na taarifa za kutosha. Hivyo, serikali na wadau wengine wanapaswa kukuza ufahamu kwa jamii juu ya usitishwaji wa 'Dental Amalgam' ili waweze kuchagua kutumia dawa zisizo na zebaki," alisema Rehani.

Alisema serikali inatakiwa isitishe matumizi pia kwa makundi mengine ambayo hayajagusswa kwa sasa, ili makundi yote ya wananchi yaguswe.

"Gabon mwaka huu imepitisha kusitishwa kwa Dental Amalgam kwa watu wote kwa kuanza utumiaji wa dawa zisizo na zebaki kwa kuziba meno yaliyotoboka inawezekana kabisa.

"Madhara ya zebaki kwa ubongo ni kuathiri uwezo wa ufahamu wa mtoto na kumfanya asichangie vizuri maendeleo ya kiuchumi hapo baadaye. Hii kulingana na taarifa za Shirika la Afya Duniani (WHO)."

Katibu Mtendaji wa TCAR, Bernard Kihiyo, alisema watu waachane na dhana kwamba kuziba meno kwa kutumia zebaki ni kudumu muda mrefu, huku madhara yake yakiwa makubwa zaidi.

# Mvua kubwa kuendelea leo, kesho TMA yahadharisha El- Nino imeanza

**Na Faustine Feliciane**

HUKU baadhi ya maeneo ya Jiji la Dar es Salaam na mikoa mingine ikikumbwa na mafuriko, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), imetoa tahadhari ya uwapo wa mvua kubwa kwa leo mpaka Jumamosi huku ikiweka wazi kuwa mvua ya El-Nino imeshaanza.

Katika taarifa yake iliyotolewa jana, TMA imetoa tahadhari ya mvua kubwa katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Pwani (ikijumuisha visiwa vya Mafia), Morogoro, Lindi na Zanzibar.

Akizungumza na Nipashe jana, Mtaalamu wa Hali ya Hewa kutoka TMA, Joyce Makwata, alisema kuwa uwezekano wa kutokea mvua hiyo ni mkubwa na athari zake pia ni kubwa.

"Athari ambazo zinaweza kujitokeza ni pamoja na mafuriko yatakayoathiri eneo kubwa, pia athari kwa usafirishaji, baadhi ya barabara kutopitika na hata vifo vinaweza kujitokeza kutokana na mafuriko," alisema Makwata.

Alisema mvua hiyo ilitabiriwa na Mamlaka hiyo hasa El- Nino ambayo tayari imeanza na kuwataka wananchi kuendelea kuchukua hatua kujihadhari.

"Wananchi waendelee kuchukua tahadhari, wale wanaoishi kwenye maeneo ya mabondeni wanashauriwa kuondoka katika maeneo hayo, lakini kwa mamlaka husika zichukue tahadhari kukabiliana na athari hasa kwenye miundombinu," alisema.

Baadhi ya mikoa ambayo ipo kwenye msimu wa mvua, El-Nino itaongeza mvua kubwa kama ilivyotabiriwa hapo nyuma.

Mvua inayoendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali nchini imeanza kuleta madhara kwa wananchi na maeneo mbalimbali kumeripotiwa uharibifu wa miundombinu, kubomoka kwa nyumba na vifo.

Mkoani Arusha kumeripotiwa kutokea vifo vya watu watano vilivyotokana na mafuriko yaliyosababishwa na mvua kubwa iliyonyesha usiku wa kuamkia Novemba 13.

Jijini Dar es Salaam mvua imekuwa kikwazo kwa baadhi ya shughuli za kiuchumi huku pia ikiathiri sekta ya usafiri kutokana na baadhi ya barabara kuharibika na kutuwama maji.

Baadhi ya mito imefurika maji na kusababisha mmomonyoko wa udongo ulioathiri kwa kiasi kikubwa makazi ya watu yaliyo karibu na mito hiyo.



Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, mkoani Lindi, Mohamed Moyo, akichungulia ndani ya moja kati ya nyumba 22 zilizobomolewa na mvua katika kijiji cha Nang'olola, Kata ya Stesheni, wilayani humo jana, wakazi zaidi ya 100 hawana makazi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Rais wa Romania kuzuru nchini leo

**Na Jenifer Gilla**

RAIS wa Jamhuri ya Romania, Klaus Iohannis, atafanya ziara ya kitaifa nchini kuanzia leo hadi Novemba 19, kwa mwaliko wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Viongozi hao watashuhudia utiaji saini wa hati za makubaliano kati ya nchi zao katika sekta za kilimo, mifugo, misitu, chakula na masuala ya uokoaji wakati wa dharura.

Taarifa iliyotolewa na Kitengo cha Mawasiliano, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, imeeleza kuwa lengo la ziara hiyo ni kukuza na kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia kati ya nchi hizo na kuibua maeneo mapya ya ushirikiano ikiwamo uwekezaji, elimu, utalii, afya na utamaduni.

Imesema Rais Iohannis na ujumbe wake watawasili leo katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) na kupokewa na Waziri January Makamba.

Kesho atapokelewa na mwenyeji wake, Rais Samia, kisha atakuwa na mazungumzo ya faragha na baadaye watashiriki katika mazungumzo rasmi kuhusu uhusiano wa nchi hizo.

Baada ya kushuhudia utiaji saini wa hati za makubaliano, viongozi hao watazungumza na waandishi wa habari kuelezea masuala muhimu yaliyojiri katika mazungumzo yao.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo ya wizara, Novemba 18, Rais Iohannis na ujumbe wake watakwenda Zanzibar kuzungumza na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi na baadaye kutembelea vivutio vya utalii ukiwamo Mji Mkongwe.

Taarifa hiyo ilisema kupitia ziara hiyo, nchi hizo zimedhamiria kuinua na kuimarisha kiwango cha biashara ambacho kimeshuka kwa miaka ya hivi karibuni licha ya Tanzania kuuza zaidi bidhaa zake nchini Romania.

Nchi hizo zimeendelea kushirikiana katika sekta ya biashara na uwekezaji na bidhaa kuu za Tanzania zinazouzwa nchini humo ni minofu ya samaki aina ya sangara, chai, tumbaku na parachichi huku Tanzania ikinunua bidhaa za mashine za umeme, vifaa vya matrekta, magari na vya matibabu.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo mwaka 2021 Tanzania iliiuzia Romania bidhaa zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 7.9 (takribani Sh. bilioni 19.8), ikilinganishwa na mwaka 2022 ilipouza bidhaa zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 4.06 (Sh.bilioni 10.3).

Romania ilinunua bidhaa zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 11.6 (Sh.bilioni 29.05), ikilinganishwa na mwaka 2022 iliponunua bidhaa zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 2.4 (Sh. bilioni sita).

Kwa upande wa uwekezaji, Romania imewekeza nchini kwenye miradi ya usafirishaji, viwanda na utalii yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 6.04 (Sh. bilioni 15) na kuzalisha ajira 89. Imewekeza Zanzibar miradi mitatu yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 7.5 (Sh. bilioni 18.8) kwa mwaka 2023 na kuzalisha ajira 64.

# Hatima hukumu ya rufani ya Sabaya leo

**Na Allan Isack, ARUSHA**

HATIMAYE hukumu ya rufani ya kesi ya unyang'anyi wa kutumia silaha iliyokuwa inamkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, na wenzake wawili, itajulikana kesho.

Hukumu hiyo, ilipangwa kutolewa jana katika Mahakama ya Rufani iliyoketi Arusha lakini ilishindikana baada ya rufani wawili kutofika mahakamani.

Mbali na Ole Sabaya, washtakiwa wengine ni Sylvester Nyegu na Daniel Mbura, ambao wote kwa pamoja walikuwa wakikabiliwa na mashtaka matatu ya unyang'anyi kwa kutumia silaha.

Jana, maofisa wa mahakama wakiongozwa na Naibu Msajili wa Mahakama ya Rufani, Abeesiza Kaleyega, mawakili wa warufani (Jamhuri) na mawakili wa wajibu rufani, walijifungia faragha kwa takribani saa 1:30 na baadaye waandishi wa habari walijulishwa kuwa hukumu hiyo imeahirishwa.

Mosses Mahuna, wakili wa wajibu rufani, aliwaambia waandishi wa habari kuwa hukumu hiyo imeahirishwa kutolewa kwa kuwa warufani wawili hawakufika mahakamani kwa kuwa wako mbali.

"Hukumu imeahirishwa kusomwa leo (jana) hadi Novemba 17, mwaka huu, kwa kuwa warufani wawili (Nyegu na Mbura), hawakufika mahakamani kwa sababu mmoja yuko Kigoma na mwingine yuko Dar es Salaam," alisema Mahuna.

Novemba Mosi, mwaka huu, Mahakama ya Rufani ilisikiliza hoja sita za waleta rufani kupinga hukumu ya Mahakama Kuu Kanda ya Arusha ya kumwachia huru Sabaya na wenzake. Walidai kuwa hati ya mashtaka ilikuwa na upungufu pamoja na kukinzana kwa ushahidi wakati wa usikilizaji wa kesi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha.

Wakati wa usikilizaji wa rufani hiyo, mawakili wa wafani waliongozwa na Wakili Mkuu wa Serikali Mwandamizi, akisaidiana na mawakili Sabina Silayo, Eliainenyi Njiro, Chivanenda Luwongo na Verediana Mlenza huku wajibu rufani wakiwa ni Mosses Mahuna, Fauzia Mustaspha, Sylvester Kahunduka na Fridolin Bwemelo.

Aidha, hoja ya kwanza na sita waliziacha kama zilivyokuwa na hoja ya tatu, nne na tano waliomba kuzikusanya kuwa pamoja ila ya kwanza waliondoa.

Wakili Sabina, alidai kwamba kwa hoja ya sita baada ya kupitia hukumu ya Mahakama Kuu, Jaji alisema shahidi wa pili wa warufaniwa hakupewa haki ya kuuliza maswali ya dodoso kwa mashahidi wa kwanza na wa pili wa waleta rufani.

Hata hivyo, alidai kuwa wameona kuwa Jaji hakujielekeza na ombi hilo kwa kuwa shahidi wa mrufani wa kwanza alipewa haki yake ya kuuliza maswali.

Vilevile, ilidaiwa kwamba Jaji wa Mahakama Kuu, hakuwa sahihi kwa kusema hati ya mashtaka ilikuwa na mashtaka matatu na kila kosa lilitakiwa kuwa kivyake.

Ilidaiwa kwa hoja ya kwanza mrufani alipewa haki yake pia kwa hoja ya pili hati ya mashtaka ilikuwa na makosa matatu na kila kosa lilikuwa linaweza kusimama lenyewe.

"Hoja ya tatu si ushahidi wa shahidi wa pili uliotumika tu kuwatia hatiani kwa kuwa kulikuwa na ushahidi na mwingine na mashahidi wengine walipata haki, hivyo Mahakama Kuu haikuzingatia ushahidi wa wengine ambao uliwatia hatiani.

"Sisi tunaona mahakama ya rufani ina uwezo wa kuchambua ushahidi kulingana na hukumu ya mahakama ya hakimu mkazi na mahakama kuu ili kupata ukweli kwa kuwa tunaona mahakama kuu ilikosea" alidai.

Mahuna,akijibu hoja hizo, kwa niaba ya wajibu rufani wote, alidai hukumu ya rufani ya kwanza ilikuwa sahihi.

Alidai hoja na kwanza na sita,wameelewa kuwa ni haki ya mtu kupewa nafasi ya kuuliza maswali ya dodoso kwa mrufani wa pili na tatu kwa mashahidi waleta rufani wa kwanza na wa pili ila hawakupewa nafasi.

"Katika mazingira haya ya mtu hasa mrufani wa kwanza na pili kunyimwa haki ya kusikilizwa kushilizwa haiko sawa.

Alidai kwa hoja ya tatu imebeba hoja nyingine ikiwamo ya kwanza hivyo kwa kuwa walipaswa kufanya mabadiliko ya hati ya mashtaka.

"Jaji wa mahakama kuu wakati akitoa uamuzi aliona kulikuwa na makosa katika hati ya mashtaka alichagua. "Kulikuwa na makosa kwenye kiasi halisi cha fedha kilichochukuliwa na valeti,lesoni na eneo la duka ambalo limeelezwa liko mbondeni ilhali liko soko kuu Arusha.

"Kosa hili la unyang'anyi wa kutumia sihala sitaweza kuthibitika vipi ilhali kuna makosa yaliyojidokeza katika hati ya mashtaka.

"Katika ushahidi mzima hakuna kokote tumeambiwa aliyeiba fedha Sh.milioni 276,9000 kwa kuwa siku ya tukio haikujulikana kama pesa zimechukuliwa hadi baada ya siku tatu kupita," alidai.

Oktoba 15, 2021, Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha, chini ya Hakimu Mkazi Mwandamizi,Odira Amworo, iliwatia hatiani Ole Sabaya na wenzake kutumikia kifungo cha miaka 30 jela.



Waziri wa Madini, Athony Mavunde (wa pili kushoto), akizungumza na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Tembo Nickel, Benedict Busunzu (kushoto), alipotembelea Mradi wa Kabanga Nickel. Wa pili kulia ni Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa na Ofisa Mkuu wa Biashara wa Benki ya CRDB, Boma Raballa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mavunde: Tembo Nickel itakavyoiweka Tanzania kwenye ramani ya dunia

**Na Mwandishi Wetu,**
NGARA

WAZIRI wa Madini, Anthony Mavunde, ameshuhudia Kampuni ya Tembo Nickel ikizindua mchakato wa ulipaji fidia kwa wananchi wanaotarajia kupisha mradi huo wa uchimbaji madini ya Nickel wilayani Ngara na kusema mradi ni wa kihistoria Kusini mwa Jangwa la Sahara, na kuwa serikali inautumia kama mfano kwenye miradi yote ya madini ya kimkakati.

Mavunde alisema hayo wilayani Ngara alipotembelea eneo la Mradi wa Kabanga Nickel, unaoendeshwa na Kampuni ya Tembo Nickel ambayo aliambatana na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa, pamoja na Kamati za Kudumu za Bunge za Nishati na Madini na Ardhi, Maliasili na Utalii.

Akizungumza na wananchi waliojitokeza kushuhudia kwenye Kijiji cha Bugarama, Kata ya Bugarama, Mavunde alisema mradi huo ni muhimu kwa manufaa ya Tanzania na serikali ni mbia ikiwa na hisa asilimia 16 kwenye kampuni ya Tembo Nickel.

"Mradi huu ni muhimu kwasababu sasa hivi dunia inakwenda katika nishati safi. Mradi huu unakwenda kuingia katika historia kusini mwa jangwa la sahara, kati ya miradi michache ambayo itakuwa na teknolojia ya kisasa ya kuchenjua makinikia haya ambayo yatachimbwa hapa. Teknolojia hii ya kisasa ya uchenjuaji haitakuwa na athari kwa mazingira na huu mradi serikali tunautumia kama kielelezo cha miradi mingine yote inayokuja ya madini mkakati, ya uongezaji wa thamani," alisema Mavunde.

Alisema madini ya Nickel, mahitahji yake duniani kwa sasa ni tani milioni 10 kwa mwaka na ifikapo mwaka 2050, yatakuwa tani milioni 150.

"Kampuni ya Tembo Nickel itakwenda kujenga kiwanda cha uchenjuaji pale Kahama, ambapo kitakuwa kinafanya kazi ya kusafisha na kupeleka katika hatua ya mwisho kabisa malighafi hii ambayo hivi sasa ina uhitaji mkubwa sana duniani," alisema Mavunde.

Waziri Silaa, alipongeza mchakato wa uhamishaji watu na makazi unaofanywa na Tembo Nickel akisema umezingatia sheria za nchi pamoja na kanuni za kimataifa jambo ambalo limeondoa malalamiko kwa wananchi.

"Utekelezaji mradi huu unaenda kutekeleza vigezo vya kimataifa (IFC), mathalani kiwango namba tano kinachohusika na utwaaji wa ardhi na uhamishaji wananchi usio hiyari ambavyo Kampuni ya Tembo Nickel imevipitisha, kwa kuzingatia viwago hivyo kumekuwa na kiwango kikubwa cha ushirikishwaji wa wananchi pamoja na uwepo wa Mpango wa Uhamishaji Watu na Makazi (RAP).

"Kazi inayoendelea hivi sasa ni kuwaonyesha wananchi fidia watakazolipwa na kusaini mikataba ya fidia zao, aidha kazi ya ujenzi wa nyumba za mfano unaendelea, kazi hizi zinafanyika kwa kasi kubwa ili kuendana na kasi ya mradi," alisema.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Tembo Nickel, Benedict Busunzu, alisema waguswa wa mradi huo wamegawanyika kwenye makundi mawili, la kwanza ni la wenye mashamba ambao hawaishi kwenye eneo la mradi ambao ni 990 na wanaoishi kwenye eneo la mradi ambao ni 349.

Alisema waguswa wote wamepewa mafunzo ya maarifa ya kutumia fedha ambao yalienda sambamba na kufungua akaunti maalum za benki zitakazotumika kulipa fidia zao.

Akizungumzia uzinduzi wa ulipaji fidia, Busunzu alisema, "hili zoezi si tukio ila ni mchakato ambao umeanza muda mrefu sana, leo ni kuonyesha hatua ambayo tumefikia katika mchakato wetu ambapo tunaanza kulipa fidia kwa wale watu ambao wameguswa na mradi pia kueleza kuwa kwa vile ni mchakato kuna mambo mengine ambayo itabidi yafanyike ili sisi kama mradi tuwe tayari kuanza shughuli zetu hapa.

"Hii ni hatua kubwa ambayo sisi kama mradi tutahakikisha kwamba tunaifanya ili wale watu watakaopisha mradi wasiondoke wamenung'unika, waondoke wamefurahi na kuhakikisha mradi unafanikiwa," alisema Busunzu.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wasanii wahamasishaji matumizi dawa za kulevya wanastahili onyo

**JUZI** Mamlaka ya Kudhibiti Dawa za Kulevya Nchini (DCEA), ilitoa mafunzo kwa wahariri wa vyombo vya habari nchini kuhusu majukumu, uelewa wa dawa za kulevya, iliwaonya wasanii wanaotumia dawa hizo na kuhamasisha kupitia nyimbo zao na mavazi yao.

Hatua ya mamlaka hiyo inatokana na kujitokeza kwa baadhi ya wasanii kuonyesha kupitia nyimbo zao wanavyotumia dawa hizo kama njia ya kuhamasisha matumizi yake.

Baadhi ya wasanii hao wengine wenye majina makubwa, inadaiwa hutumika kutangaza biashara ya dawa za kulevya kwa kuhamasisha kwenye nyimbo zao kutokana na kusikilizwa pia kupendwa na vijana wengi, wengine huhamasika kuwaiga wakitaka kuwa na mwonekano wao.

Vijana ni rahisi kurubuniwa kirahisi kutokana na akili zao kwa baadhi yao kuchukua maamuzi bila kufikiri kitu wanachofanya ni kibaya na kitawaletea madhara baadaye.

Kadhalika vijana hao huiga kwa kuangalia kwenye mitandao na kuona jinsi baadhi ya wanasanii wanavyoonyesha kwenye nyimbo zao.

Mamlaka hiyo imeonya kuwa wasanii watakaobainika kuhamasisha matumizi hayo watakamatwa na kupimwa na wakigundulika kutumia watafikishwa mahakamani bila kujali umaarufu wala ukubwa wa majina yao.

Wasanii wanachukuliwa kama kioo cha jamii hasa kwa vijana, hivyo wanapofanya vitendo vinavyopotosha, vinaharibu vijana wenzao ambao ndio tegemeo la taifa la kesho.

Nyimbo na vitendo vya wasanii zinapaswa kutoa elimu itakayowafundisha vijana wenzao kufanya vitendo vizuri katika jamii.

Kipindi cha muziki wa dansi uliposhamiri, tuliwaona wanamuziki wakitunga nyimbo zinazoelimisha jamii kufanya jambo fulani kwa manufaa ya taifa.

Kwa mfano kuna bendi moja wanamuziki wake walitunga wimbo kuhamasisha umuhimu wa kuwa na shamba ili kupata mazao bora. Nyimbo nyingine zilikuwa zikihamasisha ulaji wa chakula bora na kuvitaja vyakula hivyo ili kujenga miili yenye afya.

Pia nyimbo nyingine zilikuwa zikifundisha kuheshimu wakubwa. Lakini katika kizazi hiki cha sasa nyimbo nyingi zimejaa maneno ya mapenzi na zingine ni aibu hata kuzisikiliza au kuzitazama ukiwa umekaa na mtu unayemheshimu.

Uchezaji na vitendo vinavyoonyeshwa kwenye video za muziki wao ni wazi vinaashiria kuwa hao waliotumika kucheza watakuwa wametumia kidogo kilevi ili kuondoa aibu.

Mamlaka ya Kudhibiti Dawa za Kulevya, imesema imeshaongea na Baraza la Sanaa Nchini (BASATA) na kuwakabidhi orodha ya wasanii husika, wanaotakiwa kujirekebisha na kwamba wasipofanya hivyo hatua zitachukuliwa dhidi yao.

Wasanii ni kioo cha jamii wana mashabiki na wafuatiliaji wengi, wanapohamisha jambo linafuatwa na wengi na kwa wanachokifanya kinahamasisha matumizi ya dawa za kulevya, kupitia nyimbo zao, matendo yao na wanapokuwa jukwaani, jambo ambalo siyo sahihi bali ni kuteketeza kizazi.


Madhara ya matumizi ya dawa za kulevya ni makubwa ikiwano saratani ya utumbo, koo na kuathirika kwa mfumo wa hewa.

Serikali hutumia gharama kubwa kuagiza dawa za kutibu magonjwa hayo ambazo hazipatikani ndani ya nchi ili wananchi wake watibiwe. Pesa hizo kama zingeelekezwa kwenye mambo ya maendeleo, nchi ingepiga hatua kubwa na pengine vijana wangetafutiwa miradi ya kufanya na kupunguza malalamiko ya kukosa ajira baada ya kumaliza vyuo vya elimu yajuu.

Wasanii mtumie fursa yenu ya kuwa kioo cha jamii kwa kuelimisha vijana wenzenu, kuna wasanii ambao wamejikita kutunga nyimbo za mafundisho na bado zinapendwa na vijana na watu wazima pia.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Mwandishi Wetu

# Ni pale DAWASCO inapoingia vitani kukabili majitaka mwenyeji El - nino

**USAFI** wa mazingira ni hitaji muhimu kwa mwanadamu katika kuboresha afya na kuimarisha usalama kazini, sambamba na kutunza mazingira yanayoepuka magonjwa ya mlipuko.

Ni hatua inayohusisha utunzaji mzuri vyanzo vya majitaka, kuboresha miundombinu ya kuondosha majitaka kutoka makazi ya watu, ikiwamo mifumo ya chemba na mabomba ya kuisafirisha kwenye mifumo mikuu rasmi iliyopo.

Hapo kunatajwa kuwapo suala la elimu kwa wananchi kuhusu ulinzi na utunzaji majitaka, kwa usahihi wa utupaji taka kwenye mifumo ya kuondosha majitaka.

Kwa mikoa ya Dar es Salaam na Pwani, usafi wa mazingira ni changamoto ya muda mrefu kwenye maeneo yake mengi, hususani makazi ya wananchi yenye misongamano.

Baadhi ya wananchi wamekuwa na tabia ya kuharibu mazingira wakitiririsha majitaka kutoka kwenye karo za vyoo, wakielekezwa mitaani, hali inayoleta taharuki na uchafu.

Hapo ndiko Mamlaka ya Majisafi na Usafi Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), yenye jukumu kisheria kusimamia usafi wa mazingira, imekuwa ikijitahidi kuboresha usafi huo, kwenye makazi ya watu.

Hiyo inajumuisha kuelimisha umma madhara ya uchafuzi wa mazingira kwa kutiririsha majitaka mtaani, hali inayosababisha magonjwa ya mlipuko.

Lingine, DAWASA ilibuni na kutekeleza miradi ya kuondosha majitaka kwenye makazi ya watu, ikijumuisha Mradi wa Mfumo Rahisi wa Uondoshaji Majitaka (Simplified Sewerage System).

Huo ulitekelezwa kwenye mtaa wa Buguruni na Kisiwani, Dar es Salaam, lengo ni kupunguza utiririshaji majitaka mitaani.

**BOSI DAWASA**

Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Kiula Kingu, anasema lengo la kuboresha usafi wa mazingira wa Dar es Salaam na Pwani, ni kuhakikisha makazi yaliyo safi na salama, mbali na magonjwa ya mlipuko na athari nyinginezo.

"Changamoto ya usafi wa mazingira ni korofi katika maeneo yenye msongamano wa watu na sehemu zenye kipato cha kati na athari zake ni kutiririsha majitaka mitaani.

"kupitia miradi mbalimbali ya majitaka, tumeweza kupunguza kwa kiasi kikubwa utiririshaji wa majitaka, pamoja na kudhibiti mlipuko wa magonjwa," anaeleza Kingu.

Anaendelea: "Tumeamua kuweka nguvu kubwa kwenye eneo hili la uwekezaji katika miradi ya usafi wa mazingira, husussani kipindi hiki cha mvua za El - nino, ambazo huambatana na madhara hasa kwenye mifumo ya uondoshaji majitaka na husababisha kujaa na kuvuja kwa mitaro."

Anabainisha kuwa DAWASCO imeimarisha huduma za uondoshaji majitaka majumbani, kwa magari ya kisasa yenye uwezo mkubwa na haraka, bila kuchafua mazingira au kuharibu miundombinu.

"Upatikanaji magari haya ya usafi wa mazingira yamekuwa na ufanisi mkubwa katika kutoa huduma ya uondoshaji wa majitaka kwenye makazi ya watu, kutokana na kuwa na uwezo wa kubeba kiasi kikubwa cha majitaka pamoja kwa gharama nafuu." anaeleza Ndugu Kingu.

Bosi huyo anasisitiza kwa wakati uliopo wa mvua za Elnino, magari hayo yanatumika kukabilia mazingira machafuzi.

Pia, anawakumbusha wananchi kuepuka kutupa taka ngumu kwenye mifumo ya uondoshaji majitaka, ili kusaidia isizibe, hali inayowasafirishia kirahisi.

"Niwaombe wananchi wote kutoa ushirikiano kwa mamlaka katika kukabiliana na uchafuzi wa mazingira, wakiwa mabalozi wazuri wa utunzaji wa miundombinu ya majitaka," anasema.

Mkuu huyo wa DAWASCO anafafanua: "Kwa kutoa taarifa kwa mamlaka pindi waonapoona uharibifu wa miundombinu kwenye makazi yao, ili kuokoa hatari ya uchafuzi wa mazingira,"

Pia, anataja jitihada nyingine zilizofanyika kukabili changamoto ya majitaka mitaani, inajumuisha utekelezaji miradi ya uondoshaji uchafu huo, akitaja miradi ya majitaka Ubungo hadi Sinza; Mbezi Beach; na Buguruni, zote zinalenga mazingira.

# ‘Kilimo kizingatie mnyororo wa thamani’

**Na Christina Haule, MOROGORO**

KATIBU Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Dk. Jim Yonazi, amesema upo umuhimu wa kuzingatia kilimo kwa kuingiza masuala muhimu kuanzia uzalishaji, usambazaji, uhifadhi na utumiaji kwenye programu ya kuendeleza kilimo awamu ya pili (ASDP II) ya miaka mitano ijayo ili kuboresha utekelezaji wa masuala ya kilimo nchini.

Dk. Yonazi alisema hayo jana wakati akifungua mkutano wa wadau wa kilimo na lishe katika kuangalia maboresho ya Programu ya ASDP II (2019/2028) kwa miaka mitano ijayo baada ya kumalizika miaka mitano ya kwanza (2019-2023).

Pia alisema, progamu hiyo ni mtambuka ambayo inagusa sekta nyingi muhimu na kuwataka wadau hao kutoa mapendekezo bora ya kufanya vyema zaidi kwenye miaka mitano ijayo ya ASDP II bila ya kuingiza siasa kwa kuweka wazi ukweli.

Mhadhiri na mbobezi katika masuala ya uhandisi wa kilimo kutoka Chuo Kikuu cha Mtakatifu John Dodoma, Profesa Timothes Malenga, aliishauri serikali kutumia sera ya taifa kuondoa jembe la mkono na kuliweka kwenye jumba la makumbusho na kutumia zana za kisasa za kilimo zinazoweza kuzalisha kwa haraka na wepesi kwa kuleta tija hasa katika kuvutia vijana kwenye kilimo na kuondokana na dhana duni.

Prof. Malenga alisema, kuleta dhana bora za kilimo zinazoweza kuzalisha kwa wakati na haraka husaidia vijana wanaomaliza vyuo vikuu na vya kati kuwa njia mojawapo ya kuendeleza ufanisi katika kilimo.

Alisema wanaishauri serikali kupitia ofisi ya Waziri Mkuu kusimamia fungu la pesa linalotolewa la miradi mikakati mbalimbali ya kilimo nchini ikiwamo ASDP kwa kuleta tija ya kuzingatia mnyororo wa thamani wa kilimo nchini na kuondoa ushindani wa wizara moja kwa wizara nyingine usio na tija.

Awali Mratibu wa Taifa wa (ASDP II) inayoratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu chini ya idara ya uratibu wa shughuli za serikali, Dk. Salim Nandonde, alisema katika kikao hicho wanaangalia namna ya kujumuisha eneo muhimu lililosahaulika kama sehemu ya kuendeleza kilimo, mifugo na uvuvi kwa sababu bila ya muunganiko hakutakuwa na uendeshaji mzuri.

Alisema pia katika awamu ya kwanza ya miaka mitano ya program ya ASDP II walizingatia katika eneo la matumizi bora ya ardhi na maji, kuongeza tija na faida kwenye kilimo, biashara na kuongeza thamani na uwezeshaji wa sekta ambayo yatatolewa tathmini kuonekana walipofanya vizuri kwenye kikao hicho.

# WB yaipongeza Tanzania huduma za maji vijijini

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Rais wa Benki ya Dunia (WB), Kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika, Dk. Victoria Kwakwa, ameipongeza Tanzania kuwa mfano katika utekelezaji wa programu ya uendelevu wa huduma ya maji na usafi wa mazingira vijijini.

Tanzania imetajwa kutumia vizuri utaratibu wa malipo kwa matokeo yaani Program for Results (PforR) ambayo inatekelezwa katika nchi zaidi ya 50 na kufadhiliwa na Benki ya Dunia.

Wizara ya Maji kupitia programu hiyo imetekeleza zaidi ya miradi ya maji 1,500 ambayo imekamilika na inatoa huduma.

Victoria aliyasema hayo wakati akizungumza na Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, pamoja na Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, kwenye mkutano nchini Ethiopia.

Alisema, Tanzania ni mfano bora katika utekelezaji wa Programu ya PforR na aliomba itoe uzoefu wa mafanikio yake kwa nchi zaidi ya 23 kutoka kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika zinazoshiriki mkutano wa maji na usafi wa mazingira.

Dk. Kwakwa alisema awali Tanzania ilipata Dola za Marekani milioni 350 katika miaka mitano lakini ndani ya miaka mitatu ya kwanza, ilikuwa imefikisha maji kwa zaidi ya watu wapya milioni 4.7 vijijini katika mikoa 17.

Kutokana na mafanikio hayo, alisema Benki ya Dunia imeamua kuiongezea Tanzania Dola za Marekani milioni 300, hivyo kupanua wigo wa utekelezaji kufikia mikoa 25 na kwa sasa Sh. milioni 970 zimepelekwa katika kila halmashauri kwa ajili ya kuanza utekelezaji.

Alisema mafanikio hayo yamefungua rasmi milango ya uendelevu wa programu hiyo ambayo inafikia ukomo Julai 2025 na kufuatia hoja ya Tanzania ya kuwa na PforR awamu ya pili, WB imeonesha utayari wa kuwa na PforR Awamu ya Pili katika kipindi cha mwaka 2025 hadi 2030.



Ofisa Masoko wa Halopesa, Roxana Kadio, akiongea na waandishi wa habari jana wakati wa uzinduzi wa promosheni mpya ya wateja “Okota na Halopesa” uliofanyika jijini Dar es Salaam, kulia ni Mkuu wa Kitengo cha Biashara, Joseph Jackson. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Halotel yaja kivingine msimu wa sikukuu

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Simu ya Halotel kuelekea msimu wa sikukuu kupitia huduma ya kifedha ya HaloPesa, imekuja na promosheni ya Okota na Halopesa.

Akiongea kwenye mkutano wa waandishi wa habari jana, Ofisa Masoko wa kampuni hiyo, Roxana Kadio, alisema; “Tunafuraha kubwa kuwaletea wateja wetu promosheni hii kabambe ya Okota na HaloPesa, inayowapa wateja wetu fursa ya kujishindia fedha taslimu hadi Shilingi milioni moja, kila wanapotumia HaloPesa Lipa Hapa kupitia *150*88# au kufanya miamala mbalimbali kama kutuma pesa kwenda HaloPesa, kutuma pesa kwenda mitandao mengine, kutuma pesa kwenda benki, kulipia bili, Lipa hapa, kupitia HaloPesa App.”

Alisema, zaidi ya wateja milioni 3.5 wanaendelea kufurahia huduma zenye ubora na kwa gharama nafuu muda wowote. Kadhalika, kampeni ya Okota na HaloPesa imelenga kuwazawadia wateja katika msimu wa sikukuu kila wanapofanya miamala ya Lipa Hapa kupitia USSD na miamala mengine ya HaloPesa kupitia HaloPesa App itakayomuwezesha kuingia katika droo ya kila siku, wiki na mwezi. Aliongezea Roxana.

Kampeni ya Okota na HaloPesa ni kwa ajili ya wateja wa HaloPesa ambayo itakuwapo kwa miezi mitatu na jumla ya wateja 300 watakuwa washindi.

HaloPesa itaendelea kufikiria njia nyingine zaidi za kufanya ulimwengu wa huduma za kifedha kupitia simu kuwa bora zaidi kwa ajili ya wateja wao.

## KABWELA

Na Fadhil Mohammed



# Marekani yasaidia vifaa vya bil. 1.2/- upimaji magonjwa

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Afya imepokea msaada wa vifaa vya maabara vya zaidi ya Dola za Kimarekani 488,000 (zaidi ya Sh. bilioni 1.2) kusaidia upimaji wa vimelea vya malaria na magonjwa mengine.

Msaada huo umelenga upimaji kwa ufanisi zaidi ikiwa ni mpango wa Rais wa Marekani wa kupambana na malaria (PMI).

Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUCOHAS) kimekabidhiwa sehemu ya msaada huo kwa niaba ya vyuo vilivyoko chini ya Wizara ya Afya vinavyotoa mafunzo ya kozi ya maabara vilivyopo katika mikoa sita vitakavyofaidika na msaada huo.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mkurugenzi wa Ofisi ya Afya kutoka Shirika la Kimataifa la Misaada la Marekani (USAID) Tanzania, Anne Murphy, alisema hadubini 133 na vitendanishi vya maabara vilivyotolewa vitawezesha Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria.

Alisema vitaimarisha uwezo wa kimaabara katika uchunguzi na kusaidia utoaji matibabu ipasavyo kusaidia kuokoa maisha ya watu na kuzuia madhara ya Malaria.

Serikali ya Marekani imeipongeza Tanzania kupitia Wizara ya Afya kutokana na juhudi zake zilizosaidia kushuka kiwango cha ugonjwa huo nchini kutoka asilimia 14 mwaka 2015 mpaka asilimia nane mwaka 2022. Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, Prof. Mohamed Janabi, alishukuru kwa msaada huo uliolenga kusaidia kuendelea kupambana na kutokomeza malaria nchini.

Alisema msaada huo umetolewa wakati mwafaka kipindi ambacho serikali kupitia Wizara ya Afya imewekeza fedha nyingi ili kuboresha huduma za afya kwa kununua dawa na vifaa tiba.



Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Oryx Gas Tanzania, Benoite Araman (katikati), akielezea mchango wa kampuni hiyo katika kufanikisha jitihada za serikali za kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia kuelekea mwaka 2032, wakati wa Mkutano wa Mawaziri wa Afrika kuhusu uwekezaji kwa maendeleo ya usawa na jinsia jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na wenye Mahitaji Maalum, Dk. Doroth Gwajima na Waziri wa Jinsia, Kilimo, Sanaa na Mali Kale wa Kenya, Aisha Jumwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Menejimenti ya TRC yabanwa mkataba hali bora wafanyakazi

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

KIKAO cha Baraza Kuu Maalum la Chama cha Wafanyakazi wa Reli Tanzania (TRAWU), kimeipa siku 30 Menejimenti ya Shirika la Reli Tanzania (TRC) kuboresha mikataba ya hali bora kwa wafanyakazi.

Iwapo shirika halitatekeleza jambo hilo, chama hicho kimesema kitatangaza mgogoro wa kimaslahi dhidi ya mwajiri.

Akitoa tamko hilo la baraza baada ya kuainishwa maazimio manne yaliyopitishwa na wajumbe katika kikao kilichofanyika mjini hapa juzi, Katibu Mkuu wa TRAW, Raphael Kazyoba, alisema katika baraza limeazimia mkataba wa hali bora kwa wafanyakazi ili kuboresha maslahi ya wafanyakazi.

Alisema mkataba huo wa shirika ambao rasimu yake ilishakuwa tayari tangu Februari, mwaka huu, mpaka sasa haujafanyiwa kazi, hivyo ufanyiwe kazi kwa haraka.

Kazyoba alitaja azimio lingine kuwa ni TRC kuboresha kanuni za utumishi kuwa zina upungufu kwa kuwa hazikuzingatia mambo ya umri kazini na walioandaa hawana taaluma na utaalam wa mambo ya reli.

"Baraza kuu linaitaka menejimenti ya TRC kuutazama upya kwa kushirikiana na TRAWU ili kuzingatia mambo muhimu ya umri wa mfanyakazi awapo kazini. Azimio la tatu ni kutokuwa na imani na mkurugenzi mkuu wa TRC kutokana na kuchelewesha mchakato wa wa utiaji saini rasimu ya mkataba wa hali bora ili kuanza kutumika kwa wafanyakazi," alisema.

Katika azimio lingine, baraza lilisema halina imani na mkurugenzi wa rasilimali watu katika kushughulikia suala la mkataba huo jambo linalofifisha uhusiano baina ya menejimenti na chama cha wafanyakazi.

Kutokana na hali hiyo, baraza lilipendekeza mwajiri wake amwondoe haraka kweye nafasi yake kwa maslahi mapana ya wafanyakazi na TRC ili kuleta tija mahali pa kazi.

Kazyoba alitaja azimio la nne kuwa endapo maazimio hayo yatapuuzwa au kutochukuliwa kwa uzito, TRAWU itaendelea na hatua zaidi za kisheria ikiwamo kuanzisha mgomo mahali pa kazi.

Mwenyekiti wa TRAWU Taifa, Jacob Shindika, alisema chama hicho kinahitaji kuhakikisha wafanyakazi wanasikilizwa na kupewa haki katika maslahi yao sawa na walivyo wafanyakazi wengine nchini.

Alisema baraza kuu maalum lilitishwa kutokana na changamoto zilizojitokeza ndani ya TRC tangu mwaka 2012 ikiwamo wafanyakazi kutokuwa na mkataba wa hali bora na kwamba chama kimeandika takriban barua nne kwa menejimenti kuomba kutiwa saini kwa mkataba lakini hadi sasa hakuna kilichofanyika.

## Serikali yapongezwa kuruhusu dawa asilia

**Na Beatrice Moses**

BAADHI ya wadau wa sekta ya afya wameridhishwa na hatua ya serikali kuruhusu rasmi dawa 102 za asili kutumika kwenye mfumo wa tiba katika hospitali za umma.

Mhadhiri na Mshauri wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili (MUHAS), DK. Mourice Mbunde, amesema hatua hiyo ya serikali inachochea kukua kwa tiba ya asili na kutibu maradhi mbalimbali yanayowakabili watu watu kwa njia ya tiba lishe kwa kuwa baadhi ya dawa hizo zimetengezwa kwa viungo au chakula asili.

Akizungumzia juzi katika mafunzo kwa waandishi wa habari kuhusu tiba za asili zilivyotumika katika janga la COVID-19, alisema dawa hizo zilionyesha matokeo mazuri, ambayo yalithibitishwa na utafiti uliofanyika na kubaini usalama wa dawa hizo.

Katika mafunzo hayo yaliyoandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Dk. Mbunde alisema dawa hizo zilizoruhusiwa na serikali licha ya kutibu magojwa ya matatizo ya kupumua, magonjwa 14 yasiyoambukiza na magonjwa saba ya kuambukiza.

Magonjwa kadhaa inayotibu ni pamoja na shinikizo la juu la damu, kisukari, malaria vidonda vya tumbo, maambukizi kwa njia ya mkojo (UTI), pumu na uvimbe wa tezi dume.

Mengine ni mgoro, sundo, mba wa ngozi na nywele, bawasiri, kupoteza fahamu au kumbukumbu, usaha masikioni, mifupa kupauka na mafindo findo.

Magonjwa mengine yanayotibiwa na dawa hizo za asili ni uvimbe, tumbo la uzazi, maumivu ya meno na fizi, mba sehemu za siri za mwanamke, maumivu ya tumbo wakati wa hedhi, maumivu ya maungio na mifupa, nguvu za kiume na kuharibika mimba mara kwa mara.

Dk. Mbunde pia alisema hatua hiyo ya serikali imeonyesha kuwa ni fursa ya kiuchumi kwa kuwa MUHAS sasa inapokea watu wa kada tofauti, wakiwamo wafanyabiashara kujifunza kozi fupi.

Amina Ally kutoka asasi za kiraia alisema kuruhusiwa kwa dawa hizo ni faraja kubwa kwa kuwa ni dawa ambazo zimekuwa zikitumika na mababu na mabibi tangu zamani, hivyo ni kuendeleza utamaduni.

Akizungumzia kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa TAMWA, Florence Majani alisema waandishi wanapaswa kuendelea kujifunza mambo kadhaa kuhusu COVID - 19 Kwa kuwa ni ugonjwa ambao unatajwa au kuaminika kuwa bado upo, hivyo wanawajibika kufikisha taarifa sahihi kwa jamii ili kuepusha athari, zikiwamo za kiafya.



## Wakamatwa usafirishaji dawa za kulevya

Na Cynthia Mwilolezi,

ARUSHA

JESHI la Polisi mkoani Arusha, limewakamata watu 188, wanaotuhumiwa kwa makosa mbalimbali, ikiwamo wizi na usafirishaji wa dawa za kulevya.

Akizungumza na vyombo vya habari jana, Kaimu Kamanda wa Polisi, Mkoa wa Arusha, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP), Salvas Makweli, kati yao, wawili walikamatwa na bunda 542 za dawa za kulevya aina ya mirungi, yenye uzito wa kilogramu 298.

Alisema jeshi hilo lilifanya operesheni maalumu ya kuwasaka watuhumiwa hao kuanzia Oktoba 13 hadi Novemba 13 mwaka huu na kuwakamata watuhumiwa hao.

Alisema Novemba 12 mwaka huu, saa 3:00 asubuhi, maeneo ya Philips katika Halmashauri ya Jiji la Arusha, walifanikiwa kumkamata Gilbert Joseph (33), Mkazi wa Sinoni na Peter Waweru (33), Mkazi wa nchi jirani, wakiwa wanasafirisha dawa za kulevya.

Kwa mujibu wa Makweli watuhumiwa hao wanaendelea kuhojiwa na upelelezi utakapokamilika, jalada litapelekwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria.

Aliwaomba wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa kutoa taarifa za uhalifu na wahalifu kwa jeshi hilo ili kuendelea kuimarisha ulinzi na usalama katika mkoa huo.

"Lakini tunatoa onyo kwa baadhi ya wanaojihusisha na uhalifu, hususani dawa za kulevya, kuacha biashara hiyo ina haribu vijana wengi nchini ambao ni nguvu kazi ya taifa, kwani hawatasalimika na atakayekamatwa atachukuliwa hatua kali za kisheria,"alisema.

# Daktari bingwa ataja hatari kifafa cha pombe

Na Godfrey Mushi,

MOSHI

DAKTARI Bingwa wa Magonjwa ya Akili wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kilimanjaro ya Mawenzi, Emmanuel Kisanga, amesema watu wanaokunywa pombe kupindukia kutokana na msongo wa mawazo, wako kwenye hatari kubwa ya kupoteza maisha kutokana na kifafa cha pombe.

Amesema asilimia 90 ya visababishi vya magonjwa ya afya ya akili, vinatokana na changamoto za kisaikolojia na kuwasihi wanaopata msongo wa mawazo kutafuta msaada wa kitabibu na si pombe.

Dk. Kisanga aliyasema hayo jana alipozungumza na wanaharakati 20 kutoka Kata za Mwika Kaskazini, Mwika Kusini, Old Moshi Magharibi, Kibosho Magharibi na Kirua Vunjo Kusini, wakati wa mafunzo ya siku moja ya afya ya akili.

Mafunzo hayo ya afya ya akili, yameratibiwa na Shirika la KWIECO, linalofadhiliwa na Women Fund Tanzania Trust (WFT Trust), kupitia mradi wa jitihada za jamii katika kuzuia na kutoa taarifa dhidi ya wanawake na watoto.

"Ukipata kifafa cha pombe na usipowahishwa hospitalini unaondoka (unakufa). Wangapi mmeshawaona watu wamezimika baa? Hizo ni dalili. Ina maana kama alikunywa kupitiliza, anaweza akafia pale pale kwenye kiti," alifafanua Dk. Kisanga.

Aliwaonya vijana wanaochanganya pombe za aina tofauti na dawa za kulevya kuwa zinachangia kwa kiasi kikubwa mtu kupata kifafa cha pombe.

Aliwaelekeza watu hao kujikinga na ugonjwa wa malaria kwa kuwa kuugua mara kwa mara ugonjwa huo kunachangia mtu kupata ulemavu wa akili au ugonjwa wa akili, kwa kuwa hizo ni sababu za kibaiolojia.

Mwanaharakati Easther Temba, Mwanaharakati kutoka Mwika Kusini, alisema katika semina hiyo amejifunza viashiria na visababishi vya afya ya akili kama vile ulevi wa kupindukia, vitendo vya ukatili, mfumo wa maisha, hali ngumu kiuchumi na maisha pamoja na matumizi ya dawa za kulevya.

Mratibu wa mradi wa jitihada za jamii katika kuzuia na kutoa taarifa dhidi ya watoto na wanawake, Veronica Ollomi, alisema moja ya lengo la mradi ni kuimarisha afya ya akili ili kupunguza wimbi la vijana wasiolijenga taifa.

Alisema pia unalenga kukabiliana na ukatili dhidi ya wanawake na watoto katika Halmashauri ya Moshi kwa kuimarisha afya ya akili kwa waathirika wa ukatili wa kijinsia, na kuhimiza jitihada za jamii katika kuhamasisha usawa, kutoa taarifa kuhusu ukatili wa kijinsia na kuhimiza uwajibikaji katika huduma rafiki kwa waathirika.

Alisema ili mradi huo ufanikiwe kunahitajika watu watakaojitoa kusaidia kutoa ushauri, elimu kwa jamii na kuwaelekeza watu ni wapi wanaweza kupata huduma za afya ya akili.



Mafundi wakitoa tope lililojaa kwenye mitaro ya maji katika Barabara ya Afrika Mashariki (Arusha Bypass) na kusababisha maji kujaa barabarani kutokana na mvua inayoendelea kunyesha jijini Arusha jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Kortini madai mauaji mfanyakazi wa ndani

Na Mwandishi Wetu,

HAI

WATU wawili wakazi wa Kijiji cha Uswaa, Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Fedrick Urassa (67) na Neema Ayoo (33), wameburuzwa kortini wakikabiliwa na kesi ya mauaji ya mfanyakazi wa ndani Zuwena Bitaliho (14), anayedaiwa kufanyiwa ukatili hadi kupoteza maisha.

Akisoma hati ya mashtaka inayowakabili washtakiwa hao jana, Mwendesha Mashtaka wa Polisi, Mkaguzi Msaidizi, Nkamba Mbosela, alidai watu hao walitenda kosa hilo Oktoba 23, mwaka huu.

Kwa mujibu wa Mwendesha Mashtaka huyo, upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika. Baada ya maelezo hayo, washtakiwa hawakutakiwa kujibu chochote, kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kisheria kusikiliza shauri hilo.

Kutokana na matakwa hayo ya kisheria, Hakimu Mkazi, Jusmine, aliahirisha kesi hiyo hadi Novemba 28, mwaka huu, itakapotajwa tena mahakamani hapo.

Oktoba 26 mwaka huu, Jeshi la Polisi, mkoani Kilimanjaro, ilieleza kuwa linamshikilia mwanaume mmoja, ambaye mkewe, alitoroka baada ya tukio hilo kwa kumpiga msichana wa kazi na kitu kinachodhaniwa kuwa ni fimbo.

Kupitia taarifa hiyo, Kamanda wa Polisi, Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi (ACP), Simon Maigwa, alisema mtuhumiwa huyo na mke wake walikuwa wakimchapa na kitu kinachodhaniwa ni fimbo, maeneo mbalimbali ya mwili wake na kuacha majeraha makubwa yaliyosababisha kifo chake.

Kwa mujibu wa ACP Maigwa, baada ya kutenda unyama huo, waajiri hao walimfikisha marehemu Hospitali ya Wilaya ya Hai kama mgonjwa, huku wakitambua kuwa alishafariki muda mrefu.

"Mtuhumiwa huyo na mke wake walikuwa wakimfanyia ukatili binti huyo kwa kumchapa na kitu kinachodhaniwa ni fimbo, maeneo mbalimbali ya mwili wake na kuacha majeraha makubwa yaliyosababisha kifo chake," ilieleza taarifa hiyo.



# Madiwani wataka uchunguzi mapato mitambo ya barabara

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MADIWANI wa Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga, wamemwagiza Mkaguzi wa Ndani, Simon Minja, kufanya uhakiki wa mapato ya fedha za ukodishaji wa mitambo ya utengenezaji barabara ili kubaini uhalisia wa makusanyo yake na shughuli zinazotekelezwa na mitambo hiyo.

Mitambo hiyo ni Motor Grader, Compactor Roller, Low Bed, Tractor Hea na Excavator ambayo ilinunuliwa katika mwaka wa fedha 2014/2015 kwa Sh. bilioni 1.4 kwa lengo la kufungua mtandao wa barabara vijijini na badala yake iliishia kukodishwa kama sehemu ya chanzo cha mapato ya ndani.

Hayo yalibainishwa kwenye kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2023/2024 cha kujadili masuala mbalimbali ya maendeleo ikiwamo sekta ya elimu, afya, maji, kilimo na miundombinu ya barabara vijijini.

Diwani wa Kinamapula, Sharifu Samweli, alisema baraza lilikaa na kukubaliana mitambo iwe inakodishwa kwa makandarasi wanaohitaji kama moja ya chanzo cha mapato ya ndani, lakini makusanyo hayaeleweki hali inayowatia hofu juu ya fedha halisi inayopatikana.

Alisema taarifa ya robo ya kwanza ya bajeti ya mwaka huu inaonyesha mitambo hiyo kwa kipindi cha miezi mitano imekusanya kiasi cha Sh. milioni 15.5 fedha ambayo ni ndogo huku mitambo ikifanya kazi kila uchwao.

"Mimi nafanya kazi za ukandarasi tunalipia gharama kubwa kukodisha mitambo, kwa saa moja kuanzia kilomita 100 hadi 150 kwa gari kubeba mitambo hii tunalipia Sh. milioni 2.5, sasa hapo taarifa inaonyesha mitambo yote kwa kipindi cha miezi mitano Sh. milioni 15.5, Mwenyekiti tunaibiwa tunatakiwa kuwa wakali," alisema Michael Bundala Diwani wa Kisuke.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Hadija Kabojela, aliahidi kutekeleza agizo la mkaguzi wa ndani kukagua uhalali wa mapato ya mitambo na taarifa kuiwasilisha katika kikao kijacho na sasa wako mbioni kuvifunga vifaa vya kufuatilia mitambo (Car Track) ili kuongeza ufanisi wa usimamizi wake.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Gagi Lala, alisisitiza kamati ndogo ya usimamizi wa mitambo ishirikishwe kwenye kazi zote zinazohusisha shughuli za ukodishaji wa mitambo ili kupunguza malalamiko yasiyokuwa na tija pindi inapokwenda kufanya kazi na kumtaka mkurugenzi kutekeleza agizo hilo kwa wakati.

# GCLA yatangaza vita wauzaji vifungashio kemikali hatarishi

**Na Rose Jacob,** MWANZA

MAMLAKA ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), imetangaza kuanza operesheni ya kuwasaka wafanyabiashara wanaojihusisha na uuzaji wa vifungashio vya kemikali hatarishi ndani ya jamii.

Kauli hiyo imetolewa na Mkuu wa Kitengo cha Sheria ya Huduma za Udhibiti, Glibert Ndeoruo, wakati wa mafunzo ya siku mbili kwa wasimamizi wa kemikali Kanda ya Ziwa, yaliyofanyika jijini Mwanza.

Ndeoruo alisema kuwa vipo vifungashio ambavyo vinaruhusiwa kutumika kwa wananchi ambavyo havina madhara hivyo hatokuwa tayari kuona vifungashio vilivyo na kemikali vyenye madhara kwa jamii vinaendelea kusambazwa kinyume cha sheria.

Alisema watakaobainika kupitia msako huo watachukuliwa hatua za kisheria ikiwamo kulipa faini kuanzia Sh.milioni tano hadi 200 na kuwafikisha mahakamani kwa hatua nyingine zaidi.

Alisema kuna utaratibu wa kuteketeza vifungashio vya viwandani ambavyo ni hatarishi, baadhi ya watu wanakaidi maelekezo hayo na kugeuza vifaa hivyo kuwa fursa ya kujipatia kipato, jambo ambalo linahatarisha maisha ya watumiaji.

Mkurugenzi wa Huduma za Udhibiti, Daniel Ndiyo, alisema, mafunzo hayo yamelenga kuongeza uelewa katika kutambua mambo muhimu juu ya masuala ya kemikali.

Alisema hali hiyo itasaidia kupunguza athari zake, hususani kufahamu mikataba ya kimataifa inayohusu kemikali, sheria na kanuni za udhibiti na usimamizi wa kemikali za viwandani na majumbani.

Mshiriki wa mafunzo hayo kutoka mkoani Geita, Elizabeth Chagu, aliziomba mamlaka zinazohusika kuangalia kwa upana matumizi ya kemikali kwa kutoa elimu kwa watunzaji ili kuepusha madhara kwa kuwa wengi wao hawajui namna ya kujikinga.



Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, mkoani Shinyanga, Joseph Mkude, akipanda mti katika chanzo cha maji katika Bwawa la Songwa wilayani humo, ili kulinda vyanzo vya maji visitoweke juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Halmashauri zaombwa ajira kwa wahitimu Chuo cha Nyuki

**Na Benny Kingson,** TABORA

HALMASHAURI zote nchini zimeombwa kutoa ajira kwa wataalamu waliohitimu katika Chuo cha serikali cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki (BTI) kilichopo mkoani Tabora ili kuondoa uhaba wa wataalamu hao katika halmashauri nchini.

Ombi hilo lilitolewa juzi na wahitimu zaidi ya 240 wa ngazi mbalimbali katika chuo hicho na kueleza kuwa halmashauri za wilaya, manispaa, mikoa na taasisi mbalimbali zimekuwa na uhaba wa wataalamu hao hali inayopunguza uzalishaji wa asali na mazao mengine ya nyuki nchini.

Mmoja wa wahitimu hao, David Matandiko, alisema licha ya serikali kuwa na uhaba wa watumishi hao bado wahitimu wa masomo ya nyuki wamekuwa wakikosa fursa za ajira na wakati mwingine kushindwa kutumia walichojifunza kwa manufaa ya serikali na jamii kwa ujumla.

Matandiko alieleza kuwa kwa sasa wanatumia jengo la kisasa la kiwanda cha kuchakata mazao ya nyuki kujifunza kwa vitendo na kupata maarifa zaidi na kwamba kwao kwa kupata ujuzi wa uhakika kiuhalisia.

Mkuu wa chuo hicho cha BTI, Semu Daudi, alisema mpaka sasa kuna awamu ya 12 ya wanafunzi wanaohitimu chuoni hapo wakiwa na imani kaulimbiu 'nyuki ni hazina tuwalinde na kuhifadhi mazingira yao' itakuwa kichocheo cha idadi kubwa ya wanafunzi na jamii zao kujua thamani na faida ya kutunza nyuki.

Mkurugenzi wa kitengo cha mafunzo kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Edward Kohi, alisema asali ni bidhaa yenye soko kubwa kimataifa ikiwamo China inayohitaji tani 150,000 lakini uzalishaji kwa Tanzania bado uko chini kwa kuzalisha tani 38,000 pekee.

Alisema kwa kutambua umuhimu wa asali, mwaka 2027 kutafanyika kongamano la zao hilo la ulimwenguni jijini Arusha na kuhudhuriwa na wadau kati ya 5,000 hadi 7,000 kujadiliana mambo mbalimbali yanaohusu mazao ya bidhaa hiyo.

Alisema kupitia mradi wa kupanua mnyororo wa thamani wa mazao ya bidhaa hiyo adimu BEVAK chuo hicho kitajengewa bweni la wasichana lenye uwezo wa kuchukua wanachuo 300 na hivyo kutatua moja ya changamoto zinazoikabili.

Mkurugenzi huyo alimwagiza Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wajasiriamali Mkoa wa Tabora (TWCC), Amina Madereka, kuwaunganisha wahitimu wanawake kwenye shughuli zao ili wapate wataalamu watakaowasaidia kuchakata mazao ya asali kwenye kiwanda cha Tabora Women Processing Center.

ama

ALHAMISI NOVEMBA 16, 2023

AFYA NA MAZINGIRA





Ukurasa 12

**Mageuzi; kliniki tembezi kuwafuata waliko wenye malaria na Ukimwi**



Ukurasa 13

BINGWA AFUNGUKA UZAZI MPANGO; Orodha mambo muhimu maishani, watumiaji wajibebesha mengi



Ukurasa 14

**Dk. Bingwa: Tunayoishi nayo kifamilia, ni janga masikioni mwa watoto**

MAZINGIRA

# Karipio la Rais uharibifu wa Mto Ruvu, Pwani lilivyobeba jukumu

- Anafuatilia kwa hatua, mama atue ndoo...
- Kisa na mkasa; mifugo, kilimo umwagiliaji

**Na Mwandishi Wetu**

SURA zote za uongozi wa nchi, hazifichi ishara namna mkuu wa nchi alivyojielekeza katika sekta ya maji, kuna wakati anakuwa nayo jirani mithili ya waziri mwenye dhamana.

Hiyo inakuja, huku kinamama wakiwamo taasisi ya TGNP, mwanaharakati mkubwa wa jinsia nchini katika yale wanayoyahesabu mafanikio ya Rais Dk. Samia katika miaka yake miwili ya uongozi, ni pale anakuwa mbia wao wa kampeni 'kumtua ndoo mama'.

Kimsingi, ni hatua inayohimiza upatikanaji huduma ya maji kitaifa kuondoa shida hiyo katika umma nchini, kupata maji katika umbali mdogo. Rais Dk. Samia, hakuficha hisia zake kwa waziri mteule, Jumaa Awesu akimtamkia msimamo wake "ukinizingua, nitakuzingua." Kimsingi, ni onyo zito hata akashuhudiwa mbunge huyo wa mkoani Tanga, akiwajibikia maji kweli kweli, kukidhi mahitaji ya aliyemteua.

Baada ya wastani miaka miwili, Dk. Samia akarejesha kuridhika na mheshimiwa Awesu anavyotumika, akimpa kongole na timu yake ya kazi, alipowatamkia:

"Zamani huko nilikuwa na ugomvi na watu wa maji. Kwa sasa, watu wa maji ni marafiki zangu kweli kweli! Wizara imebadilika. Taasisi zilizoko chini ya wizara zimebadilika, kazi inafanywa kweli kweli na naomba mwendelee hivyo hivyo."



Hali halisi ya mifugo, inayotajwa kuathiri upatikanaji wa maji katika Mto Ruvu, hata Rais akakemea mwenendo huo. **PICHA: MTANDAO**

Ni ishara inayozaliwa na dhana 'ukiona vyaelea vimeundwa.' Daima Rais Dk. Samia, mbali na kueleza utekelezaji, ni mfuatiliaji wa karibu wa miradi ya maji, kukagua na hata uzinduzi wa miradi, hata kugawana majukumu na makamu wake, Dk. Philip Mpango.

Mfano hai ni kilichoripotiwa na gazeti hili wiki kadhaa zilizopita kuhusu uzinduzi mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria, katika mikoa ya Simiyu iliyofanywa mwezi Februari na Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango na kisha mkoani Singida, siku kadhaa zilizopita, ikafanywa na Rais Dk. Samia.

Katika shughuli kama hiyo kwenye Mradi wa Maji Bonde la Mto Ruvu, Rais Dk. Samia, akawa mkali baada ya kupata taarifa ya kuwapo hujuma inayotoa athari ya mtiririko wa maji katika mto huo.

Hapo inajumuisha unyweshaji mifugo, pia baadhi ya wakulima wanaotumia mifumo ya Mto Ruvu kumwagilia, akaagiza mamlaka ya mkoa kuchukua hatua kudhibiti na kufanyika tathmini mpya.

**MKOANI PWANI**

Baada ya agizo, uongozi wa mkoa Pwani ukachukua hatua kutekeleza maagizo ya Rais Dk. Samia, kusafisha bonde la Mto Ruvu ili kuwezesha upatikanaji maji kwa matumizi ya binadamu.

Mwezi kama huu, Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge akatoa taarifa kwa Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango, kuhusu hatua zinazochukuliwa na mkoa kutekeleza maelekezo ya Rais Dk. Samia.

Msingi wake, lengo likawa kuondoa upungufu wa maji kwenye bonde hilo unaosababishwa na shughuli za kibinadamu, mkuu wa mkoa akiwa na ufafanuzi kazi hiyo ilifanyika kwa kutumia helikopta: Anataja kwamba wamebaini kuwapo mifugo mingi, maji kuchepushwa, lakini kwa wakati huo baadhi ya maeneo yakarejeshwa chukuliwa kudhibiti hali hiyo.

"Tuliamua kuwaelekeza wale wote wanaotumia maji, kuendesha kilimo cha umwagiliaji kwa njia halali (wenye vibali), wasitishe kwa muda, wasio na vibali pamoja na wenye mifugo kuacha mara moja na wameacha.

"Lakini, operesheni zinaendelea na kukamata watumiaji wasio na vibali na watakaokaidi maagizo na maelekezo haya."

Kunenge akabainisha kuwa, ofisi yake ilitumia utaratibu bora wa kufanya mikutano na wadau, iliyosaidia kubaini na kudhibiti uchepushaji maji na kuzuia ukataji miti, ili kutunza vyanzo vya maji.

INAENDELEA UK.12

AFYA

# Mageuzi; kliniki tembezi kuwafuata waliko wenye malaria na Ukimwi




Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, katika uzinduzi wa kliniki tembezi kukabili magonjwa ya kifua, kikuu, Ukimwi na malaria, hivi karibuni jijini Dodoma. **PICHA: YASMINE PROTACE**

**Na Yasmine Protace**

HADI sasa nchini kuna mageuzi, kuwapo kliniki tembezi inayotajwa kuwa na mafanikio makubwa yanayowawezesha watu kupata huduma za afya haraka.

Nafasi ya kliniki hizo, imekuwa na msaada kwa wananchi wa maeneo hayo, kupata huduma za afya kirahisi. Hilo linaendana na baadhi ya familia wanaowaficha wagonjwa au kuugulia majumbani, hawafiki kwenye vituo vya afya, nao kuzifikia huduma tajwa.

Sasa panatajwa huduma za kliniki tembezi, zina msaada wa kuwaibua wagonjwa wa aina mbalimbali waliokuwa majumbani na hawapati matibabu.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, anasema kuanzishwa kliniki tembezi ni sehemu ya mapambano dhidi ya magonjwa ya kifua kikuu, hali kadhalika kuwaibua wenye maradhi kama ukimwi na malaria.

Ummy anasema, kliniki tembezi zimewekwa kutumikia mapambano dhidi ya ugonjwa tajwa. Hiyo ilikuwa katika hafla ya kukabidhi magari ya kliniki tembezi yenye thamani ya shilingi milioni 618,477,000, mjini Dodoma.

Waziri Ummy anaeleza: "Karibu asilimia 35 ya wagonjwa wa kifua kikuu bado tunao katika majumba yetu, ofisi zetu, vijiji vyetu na mitaani kwetu.

"Naamini kabisa, magari haya yatatumika katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa 'TB' kwa kuibua wagonjwa wapya, mapambano dhidi ya malaria na ukimwi."

Waziri anafafanua kuwa magari hayo yatatoa huduma za afya za kisasa katika jamii zilizo mbali, pia kutembelea masoko na stendi za magari, zikitoa huduma za upimaji afya kwa umma.

"Magari haya pia yatumike kutoa huduma za chanjo kwa watoto ambao wanapaswa kupata chanjo. Pia, yakatumike kwenye mapambano dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza," anatamka.

Waziri anaendelea: "Mtu akikutwa na changamoto, basi aambiwe aende kwenye kituo cha kutoa huduma za afya kwa matibabu zaidi."

Hapo anataja changamoto za kwenye magonjwa yasiyoambukiza ikiwamo kisukari, walio nayo wako wastani wa asilimia tisa, kati ya watu 100 wenye umri wa miaka 15 na zaidi. Vilevile, wastani wa wenye maradhi shinikizo la juu la damu, ni asilimia 25 hawajijui.

"Natoa shukurani nyingi sana kwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kujali Afya za Watanzania kwa kuendeleza ushirikiano na mataifa mbalimbali na kuja kuwekeza nchini, hasa katika sekta ya afya," anatamka.

Waziri Ummy anaitaja asasi ya kidini nchini Aga Khan, pia Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KFW), zimechangia kuwekeza kwenye sekta ya afya, kuunga mkono juhudi za serikali, chini ya Rais Dk. Samia, wakiboresha upatikaji huduma za afya nchini.

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Dk. Wilson Mahera, anataja matumizi ya magari hayo yatasaidia upatikanaji huduma za afya kwa haraka katika jamii, ambazo zipo mbali na vituo vya afya.

Pia, anasema watasimamia na kutekeleza maelekezo yote yaliyotolewa na Waziri wa Afya, Ummy, ikiwamo usimamizi mzuri na wa karibu, pia maendeleo ya mradi na shughuli zote zitakazotekelezwa na magari ya kliniki tembezi.

**MAAMBUKIZI MAPYA**

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Dk. Grace Magembe, alipoongoza ugeni wa Mfuko wa Dharura wa Rais wa Marekani wa Ukimwi, anasema maambukizi mapya ya virusi vya Ukimwi yamepungua kutoka asilimia saba, hadi asilimia 4.3.

Anasema, kasi ya maambukizi mapya ya virusi vya ukimwi imepungua kutoka asilimia saba mwaka 2003 hadi asilimia 4.3 mwaka jana.

"Tanzania imepiga hatua kubwa katika kuimarisha huduma za afya, hasa katika huduma jumuishi kwa waathirika wa dawa za kulevya na VVU" anasema Dk. Magembe.

Ni ziara inayomjumuisha, Kaimu Naibu Mratibu Mkuu wa masuala ya Ukimwi wa Mfuko wa Dharura wa Rais wa Marekani (PEPFAR), Dk. Rebecca Bunnell, wakiwa mkoani Tanga, mbele ya Mkuu wa Mkoa, Waziri Kindamba.

Dk. Magembe anasema, kupitia ufadhili wa PEPFAR Tanzania imeanzisha vituo tisa vya kutoa dawa aina ya 'methadone' kwa waathirika wa dawa za kulevya nchi nzima, vilevile huduma ya kliniki ya kutembea katika vituo saba.

"Serikali ya Marekani kwa msaada wake kupitia Mfuko wa Dharura wa Rais wa Marekani wa Ukimwi (PEPFAR), inaendelea kushirikiana katika uboreshaji huduma za afya nchini na mapambano dhidi ya virusi vya Ukimwi," anatamka Dk. Magembe.

Pia, Dk. Rebecca anaishukuru serikali kuikaribisha PEPFAR mkoani Tanga kwenye ushirikiano wa serikali kupambana na Ukimwi, pia virusi vyake, akielekeza rai mahsusi kwa Rais Dk. Samia, akimtaja anaimarisha huduma za afya nchini, huku naye akiahidi serikali ya Marekani itaendelea kushirikiana na Tanzania kuboresha huduma za Afya.

## Karipio la Rais uharibifu wa Mto Ruvu, Pwani lilivyobeba jukumu

**INATOKA UK.11**

"Kutekeleza maagizo ya Rais, niliitisha Mkutano wa Viongozi wa Mkoa ulioshirikisha Chama cha Wafugaji, Chama cha Wavunaji Mkaa, viongozi wa Bonde la Wami Ruvu na Wakala wa Huduma za Misitu.

"Ninashukuru Waziri wa Maji alihudhuria na kikao hicho, kikaweka mikakati ya kuhifadhi mazingira, kwa kutoharibu vyanzo vya maji na kuzuia ukataji haramu miti."

Kuhusu kudhibiti ukataji miti na uchomaji mkaa ovyo, Kunenge anaeleza mkoa wa Pwani umeazimia kudhibiti vyombo vya usafiri, hasa pikipiki zinazobeba mkaa, ili vijisajili na kuvifuatilia kujua wanakotoa mkaa huo.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Mkoa Kunenge, mpango uliopo sasa kutekeleza maagizo ya Rais, unajumuisha kudhibiti uvunaji mkaa kwa kupunguza utoaji vibali vya mkaa, ikiwa ni sehemu ya kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya gesi.

Upande wa mifugo, Kunenge anasema kuna changamoto kubwa ya uvamizi wa mifugo katika kipindi cha ukame.

"Viongozi kutoka mikoa yenye mifugo mingi, tumekubaliana kuwa wafugaji wabakize mifugo yao kwenye maeneo yao na itambuliwe, ili kuweka mikakati ya upatikanaji malisho na maji, huku mikakati ya kuhuisha matumizi bora ya ardhi, kuanzisha na kutumia ranchi ndogo ikiendelea.

"Makamu wa Rais alitembelea chanzo na mitambo ya maji ya Ruvu Chini, iliyopo katika Kijiji cha Kongo Kata ya Yombo Wilaya ya Bagamoyo, mkoani Pwani kujionea hali ya upatikanaji maji ulivyo kwenye bonde la Mto Ruvu, unaotegemewa na mikoa ya Pwani na Dar es Salaam," anatamka.

**ZIARA NA MAJI**

Rais Dk. Samia alipozindua Skimu ya Maji ya Kakonko – Kiziguzigu, mkoani Kigoma, inayotekelezwa na serikali kupitia Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) kwa kushirikiana na Taasisi ya Enabel kutoka nchini Ubelgiji, akaendelea kusisitiza thamani ya maji kwa umma.

Ni skimu ya shilingi bilioni nne na inatarajiwa kunufaisha kata nne za Kakonko Mjini, Kiziguzigu, Kasuga na Kanyonza zenye jumla ya vijiji 14.

Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, anasema Mradi wa Kakonko - Kiziguzigu utakapokamilika katika vijiji vyote 14 utahudumia wakazi wapatao 65,010. Nia ni kufikia wakazi wapatao 132,425 ifikapo mwaka 2042 ambao ndio kipindi cha usanifu wa mradi.

Awamu ya kwanza ya mradi imekamilika katika vijiji vya Kakonko, Itumbiko, Mbizi, Kiziguzigu, Kiyobera, Ruyenzi, Kabingo na Kasuga mkoani Kigoma, ambako kwa sasa wananchi wanapata huduma ya maji.

Mradi huo unatajwa kumeongeza upatikanaji wa maji kutoka asilimia 51 hadi zaidi ya asilimia 70, huku mgao wa maji ukipungua kutoka saa 12 hadi matano kwa siku, mipango ikiendelea kupanua mradilii huduma ya maji katika wilaya ifikie asilimia mia moja.

Kabla ya hapo akiwa mkoani Mtwara, nako akaahidi serikali kuwahakikishia wananchi wake wanafikiwa na huduma za mkoa zinawatosheleza kwa kuwa na huduma ya majisafi, salama na inayotosheleza.

AFYA

BINGWA AFUNGUKA UZAZI MPANGO:

# Orodha ya mambo muhimu maishani, watumiaji wajibebesha mengi potofu

**Na Elizabeth Zaya**



Huduma za kliniki zikiendelea. **PICHA: MTANDAO**

WATAALAMU wa afya wana mtazamo kitaalamu kwamba uzazi wa mpango ni njia muhimu kukabili na vifo vya kinamama na watoto, hususan penye ujauzito katika umri mdogo au umri mkubwa zaidi.

Ripoti ya Utafiti wa Demographia na Afya Tanzania (TDHS), iliyotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) 2015/2016, inaonyesha sababu zinazochangia vifo vya uzazi, ni kuzaa katika umri mdogo au mkubwa sana, kujifungulia nyumbani au utoaji mimba, ikionyesha takwimu kwa kila vizazi hai 100,000, kuna vifo 556.

Wataalamu wanashauri njia ya kupambana na vifo vya kinamama na watoto vitokanavyo na uzazi, ni kuzuia mimba zisizotarajiwa, kupishanisha watoto katika umri unaoshauriwa kitaalamu na kutumia njia za uzazi wa mpango kuzuia mimba.

Jamii inatajwa kukumbana na changamoto ya imani potofu na mitazamo hasi miongoni mwao.

### TABIBU UZAZI

Dk. Selemani Mbyallu, Msimamizi wa Kitengo cha Ubora kutoka Taasisi ya Marie Stopes nchini, anasema kitu kikubwa wanachopambana nacho sasa katika suala la uzazi wa mpango, ni kuhusu imani potofu.

Anafafanua imani potofu kuhusu uzazi wa mpango ndani ya jamii, ni zao la watu kukosa elimu stahiki, pia maoni potofu wanayoyopata mitaani, pia kwenye mitandao ya jamii kuhusu eneo hilo.

"Mengi yanayoongelewa mitaani au kwenye mitandao ya kijamii kuhusu uzazi wa mpango ni imani potofu, ikumbukwe kuwa, ili mtu aanze kutumia njia za uzazi wa mpango, ni lazima apewe ushauri kutoka kwa mtaalamu, atumie kwa muda gani, inafanya kazi kwa muda gani na njia gani atumie," anasema Dk. Mbyallu.

"Endapo kukatokea maudhi madogo madogo, mtumiaji hushauriwa kumuona mtaalamu hospitalini au kituo cha afya," anaeleza uzoefu wake, akiendelea:

"Kinyume chake, kinachotokea mtaani utasikia mara ukiweka vijiti vinapotea, wengine ukiweka vijiti wanasema wananenepa sana... kuna watu wanene tunawajua lakini mbona hawajaweka vijiti?"

Dk.Mbyallu anapinga dai la mtu akiweka kijiti ananenepa na hutolewa hospitalini, baada ya muda wake kwisha na wapo wanaoweza kuweka kwa mwaka mmoja au miwili na akirudi hospitali kutoa, anapohitaji kubeba mimba.

"Kuna imani potofu nyingi sana, lakini ili kumaliza hili, kuna umuhimu watu wajenge utaratibu wa kutafuta taarifa kutoka kwenye vyanzo sahihi, kwamba ukitaka taarifa za uzazi wa mpango sio kwenda mitaani, badala yake utafute kituo cha afya au kwa wataalamu wa afya," anasema Dk.Mbyallu.

Anarejea wao Taasisi ya Marie Stopes kwa kushirikiana na serikali - Wizara za Afya na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali ya Mitaa (TAMISEMI) wanaendesha miradi ya kusaidia eneo hilo la uzazi wa mpango, lengo ni kuhakikisha wanapata taarifa sahihi katika eneo hilo.

Lingine analitaja, pia wamekuwa wakizunguka kutoa elimu kupitia njia mbalimbali, ikiwamo kufanya 'mabonanza' kwenye makundi ya wajasiriamali na kwenye vikao, pia mikutano ya vijiji.

### MRATIBU AFYA MORO

Mratibu Afya ya Uzazi Mkoa wa Morogoro, Catherine Madaha, anasema njia sahihi ya kuondoa mitazamo hasi kwa jamii, ni kwa watoa huduma katika vituo vya afya kuhakikisha wanatoa elimu sahihi ya uzazi wa mpango kwa wananchi.

Anashauri haja ya kuongezwa nguvu ya utoaji elimu, kuepusha watu wengi kujazwa na fikra potofu, kuhusu njia hizo za uzazi wa mpango.

"Imani potofu tunaweza kuzimaliza sisi watoa huduma katika utoaji elimu kuhusu njia hizi, kwa kutoa elimu kiundani na kuwapa wateja nafasi ya kuchagua njia sahihi za kutumia," anasema Madaha.

Anaendelea: "Kama ni sindano, vijiti, mipira na kitanzi na tuwaelezee njia moja baada ya nyingine, faida zake pamoja na maudhi yake madogo madogo.

"Wakati mwingine, mitazamo hasi inakuja kutokana na mtu mmoja ambaye amepata maudhi madogo madogo katika mwili wake na kuanza kupotosha wengine.

"Ni kwa kuchukulia moja kwa moja kwamba njia hizo sio nzuri bila kufahamu kwamba huenda shida ni mwili wake tu ambao umepokea njia aliyoitumia kwa hali tofauti," anaeleza Madaha.

Hapo ana ushauri kwamba, kabla ya kuanza kumpatia mteja njia hizo za uzazi wa mpango, ni vema akapimwa na kujiridhisha njia sahihi inayoweza kumsaidia, pasipo kumletea maudhi madogo mwilini.

"Ila wapo watu ambao wanadanganyana mitaani kabisa kuwa, labda ukiwa na ujauzito, ukaenda kituo cha afya na kupewa njia ya uzazi wa mpango iwe kijiti, sindano au kitanzi eti mimba inatoka.

"Niwaambie tu kwamba, hakuna njia yoyote ya uzazi wa mpango inayoweza kutoa mimba wakati imeshaingia," anatamka Madaha.

### MAONI YA WALENGWA

Amina Jabiri, mkazi wa Kimara, Dar es Salaam, anasema kwa mara ya kwanza aliposikia huduma ya uzazi wa mpango, akapatwa na hofu, kwa sababu amekuwa akiwasikia watu mtaani wanasema ina madhara.

Katika ufafanuzi wake, anasema akasikia mitaani kwamba kutumia uzazi wa mpango kama kuchoma sindano, kuna uwezekano wa kuingia hedhi mfululizo.

Hata hivyo, anasema kinyume chake alipoenda kwenye kituo cha afya kupata elimu, akagundua kupotoshwa na sasa hana hofu na uzazi wa mpango.

"Nashukuru kupata elimu hii, imenifungua sana akili na naamini kwa sasa nitafanya kazi zangu vizuri na nitamlea mtoto wangu vizuri hadi muda nitakaotaka kuongeza mtoto mwingine.

"Kabla ya kufika katika kliniki, nilikuwa natumia njia ya uzazi wa mpango wa kalenda, lakini ilinishinda na nikaona bora nitumie hizi nyingine," anasema Amina.

Juma Hassan, Mkazi wa Tabata, Dar es Salaam, anasimulia alivyotishika na maneno ya mtaani kuhusu matumizi ya uzazi wa mpango, akinena:

"Yaani ukitaka uchanganyikiwe kabisa kuhusu uzazi wa mpango, ukubali kusikia ya mtaani, yana vitisho vingi mno! Kila mtu huwa anazungumza lake kuhusu mambo haya.

"Wengine walikuwa wanasema ukitumia kondomu, sijui zina vimelea...sijui mama anaweza kupata shida kwa mlango wa uzazi... maneno ni mengi kiasi kwamba ukisikia mpaka unaogopa.

"Lakini, nilipobahatika kupata elimu, ndio nikaelimika na kubaini kwamba yanayozungumzwa mitaani ni uongo, wote wanaozungumza hawajui, wanadanganyana tu.

"Kwa kweli mimi siku hizi nikisikia wanapotoshana nawaambia ukweli na huwa sisiti kuwashauri waende kupata ushauri kwa wataalamu wa afya badala ya kuendelea kudanganyana.

'Hata mwanangu nilimwelimisha kuhusu hili, kwa hiyo anafahamu kabisa kwamba endapo atajihusisha na mapenzi bila kinga kuna mawili, kupata ujauzito au magonjwa."

> **"Hata mwanangu nilimwelimisha kuhusu hili, kwa hiyo anafahamu kabisa kwamba endapo atajihusisha na mapenzi bila kinga kuna mawili, kupata ujauzito au magonjwa.**

AFYA

# Dk. Bingwa: Tunayoishi nayo kifamilia, ni janga masikioni mwa watoto wetu

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

- Zimo kutumia pamba, mafua, muziki…
- Uchafu wake dawa; mafuta kuku sumu

MASIKIO ni miongoni mwa milango ya fahamu mwilini mwa binadamu, hivyo yanapkuwa na madhara humkosesha mhusika hitaji muhimu kwa jinsia na umri wote.

Inatajwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano wanapopatwa na athari, inahatarisha ukuaji wao kiafya.

**DAKTARI BINGWA ANENA**

Bingwa wa Masikio, Pua na Koo wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara, Dk. Athanas Budodi, anasema magonjwa ya masikio yanasababishwa na vitu vingi.

Anataja sababu za asili kuzaliwa nayo, maambukizi, ajali na mifumo ya fahamu, huku, dawa nazo zinachangia kuathiri mfumo wa masikio kwa watoto. Mengine ni magonjwa yanayomtokea mtu sikio la nje, kati au ndani.

Mtaalamu huyo anasema, chanzo kwa watoto wachanga zaidi ni ya kurithi kwa wazazi wakati wa ujauzito, hasa mama asipohudhuria kliniki vizuri, mtoto anaweza akapata shida hiyo, kwa magonjwa kama virusi vya rubella, pia kaswende.

"Mtoto akiwa tumboni anaweza kuharibika masikio au akazaliwa na tatizo la masikio na ikamsumbua,"anasema Dk. Budodi

Chanzo kingine anakitaja ni magonjwa ya kuambukiza fangasi masikioni, puani na kooni pia matumizi ya pamba wazazi kusafisha masikio kunasababisha tatizo la masikio kwa watoto, eneo linaloathirika ni sikio la nje.

Daktari huyo anawatahadharisha wazazi wengi wanaodhani nta ni uchafu, kumbe inajitengeneza yenyewe kuzuia wadudu wanaotembea.

Dk. Budodi anasema nta ina tindikali, inayoua wadudu waingiao, hivyo hakuna sababu mzazi au mlezi kuziondoa kwenye masikio ya mtoto.

Anashauri mtoto anapougua mafua, hapo masikio nayo yanakua hatarini kwa wadudu watokao kwenye pua, kwenda sikio la kati.

Vilevile, anataja watoto wengi wanaangukia hatari ya shida masikioni, akitumia takwimu kwamba kwa wiki Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara, inapokea watoto chini ya miaka mitano idadi 10 hadi 20.

Mtaalamu huyo anataja lingine ni kelele inapozidi kama vile muziki, nayo ni chanzo cha masikio ya mtoto kuharibika, akishauri kuwapo sauti ya muziki wastani, kutetea usalama wa sikio.

Hapo daktatri bingwa anakumbusha hata tabia ya kupiga vibao mtoto ni hatari kubwa sikio la mtoto kuharibika, hasa penye ngoma kupasuka, mtoto anakuwa kiziwi.



Mtoto akipata tiba ya masikio. **PICHA ZOTE: MAKTABA**

> **Kipindi cha masika ndicho watoto wengi wanaongezeka kutokana na kupata mafua, akitahadharisha ni kipindi mkoani Manyara, wapo watoto wanaweka maharage au mbaazi masikioni.**

Vilevile anasema, kipindi cha masika ndicho watoto wengi wanaongezeka kutokana na kupata mafua, akitahadharisha ni kipindi mkoani Manyara, wapo watoto wanaweka maharage au mbaazi masikioni.

**UELEWA WA WAZAZI**

Dhana ya Dk. Budodil inapokewa na Joyce Tarimo mkazi wa kijiji cha Bermi, Babati, anayekubali kuweka maharage masikioni watoto wanopoyachezea, huku akitaja shida nyingine ni sabuni wanazoogeshwa.

Hata hivyo, katika kile kinaonyesha bado kuna elimu duni, mkazi wa kijiji cha Kiongozi, Mwajuma Hamis anatetea adhabu kumchapa vibao mtoto au burudani ya sauti kubwa ya muziki, kwamba haiathiri masikio ya mtoto, akikiri kwa Nipashe, amtendea hayo mwanawe.

Mkazi wa Mtaa wa Mji Mpya, Huruma Mathayo, anakiri kupiga muziki kwa sauti kubwa na hakufahamu athari zake, hasa kwa watoto.

Mkazi mwingine wa Mtaa wa Maisaka 'A', Paul Ezekiel, ana mtazamo wake, aliyoamini awali kwamba jambo pekee linalomuathiri mtoto maji yanapomuingia akiogeshwa.

**SULUHISHO LA DAKTARI**

Dk. Budodi anahimzia wazazi wawahishe watoto hospitali na wasiweke mafuta ya kuku wanaomamini ni tiba, ila hayawasaidii.

Pia, anakemea kukimbilia katika maduka ya dawa kununua dawa, inaweza kuwapa mwelekeo hasi, akifafanua kuwa kuna ugonjwa wa kufanyiwa upasuaji, pia wa kuwekewa dawa au kutumia dawa za kawaida, daktari ndiye mthibitishaji usahihi wa tiba.



Bingwa wa Tiba ya Masikio, Pua na Koo wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara, Dk. Athanas Budodi.

Kingine, anashauri wazazi au walezi wasiwapige makofi watoto, inahatarisha masikio yao, hata mtoto akaangukia maisha anajitenga na wenzake, kukosa usikivu na kushindwa kuelewa darasani.

Anafafanua kuwa, mtoto mwenye shida sikioni awahishwe hospitali, maana anayechelewa kuna wakati tiba yake analazimika kuwekewa kipandikizi cha kumuwezesha kusikia, ambayo gharama yake ni kubwa, kati ya Sh. milioni 30 hadi milioni 100.

**WADAU TIBA**

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Misheni Dareda, Manyara Dk. Joseph Lorry, anasema masikio yana matatizo mengi na anakiri kuwapokea watoto wenye shida hiyo, baadhi wanawapatia rufani kwenda Hospitali ya Kanda ya KCMC, mjii Moshi.

Anaeleza kuwa, watoto wanaathirika kupitia hali ya hewa kama mafua, tatizo likiwa kubwa wanawasiliana na mtaalam wa masikio, pua na koo anayefika kumhudumia mgonjwa wao.

Kuhusu sauti kubwa, anatamka: "Zina viwango vyake ambavyo vinatakiwa kupunguzwa, ili kumpa usikivu mtoto au mtu yeyote anayesikiliza."

Ni eneo ambalo hata serikali imeingilia kati hivi karibuni kuchukua hatua, Dk. Lorry naye akitaja shida nyingine ya sikio inaathiri ukuaji wa mtoto unaobaki kimwili, lakini si wa kisaikolojia; kujifunza, mawasiliano na kuchangamana kijamii.

Msimamizi wa Miradi ya Malezi, na Maendeleo ya Awali ya Mtoto kutoka Shirika la Children Incrossfire (CIC) Frank Samson, anasema hatua za awali za ukuaji mtoto ni muhimu kutambua mtoto tatizo lake la masikio na kulifanyia kazi.

Anadokeza, mtoto mwenye shida hiyo anashindwa kutamka maneno mengi na anaathirika kwenye ukuaji, akishindwa kujieleza na kujitetea.

**RIPOTI KIMATAIFA**

Ripoti ya Shirika la Afya Duniani (WHO) ya Machi 3 mwaka 2021 inatahadharisha kufikia mwaka 2050 takribani watu bilioni 2.5 duniani, wataishi na upungufu wa uwezo wao wa kusikia, iwapo hatua hazitachukuliwa mapema.

Ripoti inasema wastani wa mtu mmoja kati ya watu wanne watakuwa wanakabiliwa na tatizo la usikivu, huku watu milioni 700 watahitaji kutumia vifaa vya kusikiia au tiba ya masikio na huduma nyinginezo.

Pia, Ripoti ya WHO Machi mwaka huu, inaeleza kila watoto watatu kati ya watoto wanne wanapofikisha miaka 15 ya kuzaliwa, wanakuwa wamepata angalau mara moja au zaidi maambukizi ya magonjwa ya masikio na yasipopatiwa tiba, yatasababisha matatizo ya muda mrefu masikioni, hata kutosikia.

WHO imeweka viwango vipya vya sauti ambavyo ni wastani wa kiwango cha juu kisizidi 100 katika kipimo cha sauti, kuwapo mfanyakazi anayefuatilia kiwango cha sauti kisichozidi 100.

Vingine ni kuwapo vifaa vya kudhibiti sauti kuenea nje ya eneo husika, ili usikivu usigeuke vurugu kwa umma walioko kwenye utulivu wasiopenda kelele.



## PM mgeni rasmi maadhimisho Siku ya UKIMWI

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi kwenye kilele cha maadhimisho ya Siku ya UKIMWI Duniani kitakayofanyika kitaifa Desemba mosi, mwaka huu mkoani Morogoro.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Jenister Mhagama, alisema hayo jana jijini hapa, kwenye mkutano wake na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho hayo mwaka huu.

Alisema wadau wa kitaifa na kimataifa chini ya uratibu wa TACAIDS wanaendelea na maandalizi kwa ajili ya kutoa huduma muhimu wakati wa maadhimisho na kwamba kwa kawaida siku hiyo huadhimishwa ndani ya wiki moja.

Alisema shughuli mbalimbali zinazohusu utoaji wa taarifa za udhibiti wa VVU na UKIMWI zitafanyika kuanzia katika wiki hiyo inayoanza Novemba 24, hadi siku ya kilele ya Desemba 1, mwaka huu.

"Mikoa yote nchini imeelekezwa kuandaa na kuadhimisha siku hii, kupitia Ofisi ya Rais TAMISEMI, natoa wito kwa wakuu wa mikoa wote nchini kusimamia utekelezaji wa shughuli hii kwa kushirikiana na wadau wa kudhibiti VVU na UKIMWI walioko kwenye mikoa yao," alisema.

Aidha, alisema kuwa huduma za VVU na UKIMWI zinaendelea kutolewa kwa kiwango cha kuridhisha na upimaji wa hiari na utoaji wa dawa za ARV umekuwa na mafanikio makubwa kwa kuzingatia kigezo cha malengo ya 95 tatu.

"Hii inamaana kuwa asilimia 95 ya watu walio na maambukizi ya VVU wawe wametambua hali zao, asilimia 95 ya wale wanaotambua kuwa wanaishi na VVU wawe wanatumia dawa kupunguza makali za ARV na asilimia 95 ya wale wanaotumia ARV wawe wamefubaza VVU mwilini.

"Kipimo cha utendaji wetu katika kufikia malengo hayo tutakipata Desemba 1, 2023 baada ya kutangazwa na mgeni rasmi kufuatia kukamilika kwa utafiti wa viashiria vya VVU na UKIMWI wa mwaka 2022/23 ambao utatoa picha ya hali halisi ilivyo sasa," alisema.

Alitoa wito kwa wananchi na wadau wote kushirikiana katika kupanga na kutekeleza shughuli za kudhibiti VVU na UKIMWI kwa kuzingatia vipaumbele na mahitaji ya mahali walipo.

Kadhalika alitaja maeneo yanayohitaji msukumo zaidi katika mapambano hayo kuwa ni watoto, vijana na kwamba kwa kufanikiwa katika hilo Tanzania itakuwa imetimiza ndoto ya kumaliza VVU na UKIMWI ifikapo mwaka 2030.

Vilevile, alisema serikali inaongeza msukumo na vipaumbele kuimarisha afua za VVU na UKIMWI kwa vijana kwani takwimu zilizopo zinaonesha kundi hilo linachangia maambukizi mapya ya VVU kwa asilimia 40 hivyo kulifanya kuwa kwenye hatari kubwa.

# NIRC yatahadharisha wananchi kuvamia eneo mradi umwagiliaji

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

TUME ya Taifa ya Umwagiliaji (NIRC) imesema mradi wa skimu ya umwagiliaji ulioko Kijiji cha Msingi, Kata ya Msingi, wilayani Mkalama uko hatarini kupotea kutokana na wananchi kuvamia eneo hilo kujenga nyumba pamoja kufanya shughuli za kilimo.

Aidha, ilisema licha ya serikali kuwekeza zaidi ya Sh. bilioni 34 kuutekeleza mradi huo lakini unaweza usifike mahali popote kwa kuwa wananchi wamebadilisha matumizi ya eneo hilo kwa kuweka makazi ya kudumu.

Mkurugenzi wa NIRC, Raymond Mndolwa, aliwaeleza jana wabunge wa Kamati ya Bunge ya Bajeti walipotembelea mradi huo kwa ajili ya kujionea maendeleo ya ujenzi ambao ukikamilika unatarajiwa kuwanufaisha zaidi ya wakazi 12,000 wa vijiji vinne vilivyopo Kata ya Msingi.

"Wananchi wameanza kujenga nyumba na sasa tumeanza kupoteza eneo la kilimo, uwekezaji uliofanyika thamani yake ni kubwa katika eneo hilo, hivyo eneo la kilimo lazima libakie vinginevyo manufaa ya uwekezaji huu hayatapatikana," alisema.

Mndolwa aliwaomba viongozi wa serikali ya wilaya na mkoa waingilie kati suala hilo kwa kuwazuia wananchi wasiendelee kujenga mashambani kwani Sh. bilioni 34 zilizotolewa na serikali kwa ajili ya mradi huu ni fedha nyingi.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Bajeti, Daniel Silo, alisema miradi ya umwagiliaji inayotekelezwa ni kwa maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan ambaye anataka kuleta mapinduzi kwenye sekta ya kilimo ili kuongeza uzalishaji kwa wananchi na pato la taifa kwa ujumla. Silo alitoa rai kwa wananchi wasijenge kwenye eneo la mradi hasa kwenye mashamba yanayotarajia kulimwa kwani mradi huo ukikamilika utawanufaisha wao kwa kulima zaidi ya mara moja kila mwaka.

Aliiomba Wizara ya Kilimo hasa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji isimamie huo mradi ukamilike kwa wakati kwani nia ya Rais ni kuleta mapinduzi kwenye sekta ya kilimo, kila mwenye jukumu la kusimamia afanye hivyo ili ikamilike kwa wakati.

Naibu Waziri wa Kilimo, David Silinde, alisema mradi huo utakapokamilika utaongeza pato la wananchi, halmashauri na usalama wa chakula nchini kwa sababu wakulima watakuwa wanavuna zaidi ya mara mbili kwa mwaka.

Aliwataka wananchi waondoke katika eneo hilo ili waiache serikali itengeneze miundombinu ya mradi huo kwani lengo ni kuondokana kwenye kilimo cha kienyeji kuja kwenye kilimo cha kisasa chenye tija.



Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe (wa pili kushoto), akiangalia moja ya malighafi inayotumiwa na Kiwanda cha Mbolea cha Itracom Fertilizers Ltd, eneo la Nala, jijini Dodoma jana. Wengine ni baadhi ya viongozi wa kiwanda hicho. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Raia wa Burundi waiangukia serikali iwape vibali wenza wao

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

RAIA wa nchini Burundi wanaofanyakazi katika kiwanda cha mbolea cha Itracom mkoani hapo, wameiomba serikali ya Tanzania kuwasaidia wenza wao vibali vya kuishi hapa nchini ili kupunguza gharama za maisha.

Wafanyakazi hao walitoa ombi hilo mbele ya Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, wakati wa mkutano wake na watumishi wa kiwanda hicho uliofanyika jana jijini hapa.

Kiongozi wa wafanyakazi hao kutoka Burundi, Erakoze Biyenven, aliomba serikali ya Tanzania kuwasaidia wenza wao vibali vya kuishi hapa nchini ili kupunguza gharama za maisha.

"Mheshimiwa Naibu Waziri sisi wafanyakazi kutoka Burundi wapo waliokuja huku na tayari tulikuwa na familia zetu huko Burundi tunaomba serikali ya Tanzania itusaidie vibali vya hawa wenza wetu kuishi hapa nchini," alisema.

Biyenven alisema kati ya wafanyakazi hao wapo waliooa na wengine wameolewa na wenza wao wamekuwa wakipewa vibali vya muda mfupi na kurudi hivyo wanaomba kusaidiwa kukaa hapa nchini ili kupunguza gharama za maisha.

Kadhalika alisema wamekuwa wakitumia gharama kubwa kwa kuendesha maisha kwa familia zilizopo huko na hapa wanapoishi.

"Sisi tunavibali vya kuishi hapa tayari lakini tunaomba na hawa wenza wetu wasaidiwe hivyo vibali ili kuishi pamoja na familia zao tunazofanyakazi kwenye kiwanda hichi cha Itracom," aliongeza.

Awali Mjumbe wa Bodi ya Kiwanda cha Mbolea cha Itracom, William Ngeleja, alisema kiwanda hicho kitakapo kamilika kitakuwa na uwezo wa kuzalisha mbolea tani milioni moja.

Ngeleja alisema aina ya mbolea inayozalishwa hapo ni fomi ambayo kwa ajili ya kukuzia na kupandia mazao zaidi ya aina 14 yaliyofanyiwa utafiti na wataalamu wa kilimo nchini.

Aliongeza kuwa kwa mujibu wa wataalamu wa kilimo nchini mahitaji ya mbolea nchini ni zaidi ya tani 700,000 lakini wao watakuwa na uwezo zaidi na nyingine itauzwa nje ya nchi.

Pia alisema mbolea ya fomi inayozalishwa na kiwanda hicho cha Itracom Fertilizers Limited ina uwezo wa mimea kufyonza virutubisho toka ardhini kupelekea kuongezeka kwa mazao



## Kizimbani kukutwa na noti bandia

Na Nebart Msokwa, MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, linawashikilia vijana wawili kwa tuhuma za kukutwa na noti bandia wakizitumia kununulia bidhaa mbalimbali kwa wafanyabiashara hali ambayo inadaiwa kuhatarisha uchumi wa nchi.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Jeshi la Polisi, Benjamin Kuzaga, aliyasema hayo alipozungumza na waandishi wa habari ofisini kwake kuhusu operesheni mbalimbali zinazotekelezwa na jeshi hilo.

Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni James Mwamatepela (29) na Wille Mwandwani (23) wote wakazi wa Kijiji cha Ngyekye wilayani Kyela ambako ndiko walikokutwa wakizitumia noti hizo bandia.

Kamanda Kuzaga alisema vijana hao walikutwa na noti bandia 42 za Sh. 10,000 ambazo sawa na Sh. 420,000 na kwamba walikuwa wanawaaminisha wananchi kuwa ni fedha halali.

"Watuhumiwa walikamatwa Novemba 11 mwaka huu saa 8:00 mchana, ilikuwa ni sehemu ya mwendelezo wa misako mbalimbali inayofanywa na maofisa wetu kwenye maeneo mbalimbali ndani ya mkoa wetu," alisema Kamanda Kuzaga.

Aliwataka vijana mkoani humo kujikita kwenye shughuli halali za kujiingizia kipato badala ya kufanya shughuli haramu kwa maelezo kuwa jeshi hilo litaendelea kuwachukulia hatua kali.

Hata hivyo Kamanda Kuzaga aliwataka wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa jeshi hilo kwenye makabiliano dhidi ya wahalifu na uhalifu ikiwamo watengenezaji na wasambazaji wa fedha hizo bandia kwa kutoa taarifa za siri.

# CCM 'kuwatema' watakaokiuka utaratibu wa uchaguzi Mbeya

Na Nebart Msokwa, MBEYA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, kimesema kitawachukulia hatua wanachama wake waliochukua fomu za kuwania nafasi ya uenyekiti wa chama hicho mkoa, ambao watakiuka taratibu za uchaguzi ikiwa pamoja na kuwaondoa kwenye mchakato.

Uchaguzi huo unafanyika kwa lengo la kuziba nafasi iliyoachwa na aliyekuwa anaishikilia kwa takribani miezi 11, Dk. Stephene Mwakajumilo, ambaye aliteuliwa hivi karibuni na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kuwa Mkuu wa Wilaya ya Nanyumbu mkoani Mtwara.

Katibu wa Siasa, Itikadi na Uenezi wa Chama hicho Mkoa wa Mbeya, Christopher Uhagile, alitoa tahadhari hiyo jana alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu mwenendo wa uchukuaji wa fomu za kuwania nafasi hiyo.

Alisema moja ya vitu ambavyo watia nia hao wamezuiliwa ni pamoja na kuanza kufanya kampeni mapema kwa kuwa kinyume na taratibu za uchaguzi wa ndani ya chama hicho.

"Tumekuwa tukisisitiza mara kwa mara na kuwakumbusha wanachama wetu kuzingatia taratibu hizi, sasa nawakumbusha tena kwamba siku ikifika hatutaangaliana usoni, tutachukua hatua kwa mujibu wa taratibu za chama chetu," alisema Uhagile.

Katika hatua nyingine Uhagile alisema wanachama wa chama hicho waliokuwa wamejitokeza kuchukua fomu za kuomba ridhaa ya kuwania nafasi hiyo wamefika 30 huku zikiwa zimebaki saa chache muda wa kuchukua na kurejesha ufike.

Alisema kati ya wanachama hao waliojitokeza 25 ni wanaume na watano pekee ni wanawake na hivyo akawataka wanachama wa chama hicho wa makundi yote wanaowiwa kuwania nafasi hiyo kujitokeza kuchukua fomu.

Mmoja wa waliochukua fomu, Amani Kajuna, ambaye aliwahi kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa chama hicho Mkoa wa Mbeya, alisema anatamani kukiongoza chama hicho ili kutimiza haki yake ya kikatiba ya kuchagua na kuchaguliwa.

Alisema yeye maisha yake yote amekuwa akitumika ndani ya chama hicho na kwamba alipokuwa Mwenyekiti wa UVCCM alifanya kazi kubwa ya kukijenga chama na hivyo ikitokea akachaguliwa kushika nafasi hiyo ya juu atatumia uzoefu.

"Mimi nilishakuwa Mwenyekiti wa UVCCM katika Mkoa huu na pia nilikuwa Mwenyekiti wa Seneti ya vyuo na vyuo vikuu vya mkoa huu, kwa hiyo nina uzoefu wa kutosha kwenye chama hiki," alisema Kajuna.

Aliwataka vijana wengine wa chama hicho kujitokeza kuomba kugombea nafasi hiyo kwa maelezo kuwa kundi hilo ni muhimu kwa ajili ya kukijenga chama na kukitumikia kwa muda mrefu zaidi.

Kwa mujibu wa kalenda ya uchaguzi wa chama hicho leo ndio siku ya mwisho kuchukua na kurejesha fomu ili kupisha michakato mingine kuendelea.



Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (Uchumi na Sera za Fedha), Dk. Yamungu Kayandabila (kulia) akijadiliana jambo na Mkurugenzi wa Masoko ya Fedha za Kigeni wa benki ya Absa, Esther Maruma (wa pili kulia), baada ya uzinduzi wa ripoti ya Absa ya Viashiria vya Masoko ya Fedha Afrika ya mwaka 2023, jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa benki hiyo, Paul Makanza (kushoto) na Mkurugenzi wa Sheria na Malalamiko wa Absa, Irene Sengati-Giattas. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ugumu wa maisha chanzo ajira kwa watoto

Na Elizabeth John, NJOMBE

UGUMU wa maisha umetajwa kuwa moja ya sababu ya watoto mwenye umri wa kuanzia miaka 7 hadi 13 kujihusisha na kazi ya kujiingizia kipato hasa kuuza maandazi na matunda mjini Makambako mkoani Njombe.

Wakizungumza na Nipashe wakazi wa Mjini Makambako walisema sababu kubwa ya changamoto hiyo ni kutokana na watoto hao kulelewa na mama pekee au bibi.

Agrey Ndanzi alisema kuwa watoto hao kujihusisha na biashara hizo kwa muda mwingi badala ya kusoma italeta adha kubwa katika maisha yao hapo baadaye.

"Tatizo lipo kwenye jamii, tukiamua leo hii mtoto anapita nauza bagia tunamshika tunamuuliza unatoka wapi halafu tunamrudisha nyumbani tunaweza kukomesha lakini wakati mwingine mzazi unarudi saa tatu saa nne usiku uelewi watoto wamekula nini kwa hiyo watoto lazima wawe wazururaji," alisema Ndanzi.

Naye Pascal Shauri aliiomba serikali kupitia ustawi wa jamii kukabiliana na hali hiyo na kuhakikisha watoto wote wanapelekwa shule badala ya kuuza matunda na maandazi mitaani.

"Hii ni changamoto kubwa katika jamii ninachokiona mimi ni ugumu wa maisha na matatizo mbalimbali lakini utambue kuwa wazazi hawa kwa watoto waliowengi wanatoka kwa mzazi mmoja, wengine wanalelewa na mabibi zao," alisema Shauri.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Kanda ya Kusini, Siphael Msigala, alikiri kuwapo kwa watoto wengi wanaofanya kazi ya kuuza matunda na maandazi katika mji wa Makambako na kueleza kuwa hali hiyo itasababisha watoto wengi wasipende shule kutokana na kuanza kushika fedha mapema.

"Nakutana na watoto wadogo wameshika vindoo wanauza bagia, wanauza vitumbua, wanajishughulisha na biashara, kwa hiyo tatizo ni kubwa, kwanza sisi wazazi tutambue kwamba kila mtoto ana umri wake wa kufanya biashara na kila jambo kwa wakati wake," alisema Msigala.

Naye Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya Mji Makambako, Rejis Ng'itu, alisema kuwatumikisha watoto kwenye shughuli za kibiashara ni kosa kisheria na aliwataka wazazi kutowaruhusu watoto wao kufanya kazi hiyo kwani zinahatarisha usalama wao.

"Ni kweli changamoto ipo hasa katika kipindi hiki ambacho wanafunzi wapo nyumbani baada ya kumaliza masomo yao ya elimu ya msingi kwamba watoto wengi utakuta wazazurura au wanafanyishwa kazi ambazo sio msingi," alisema.

Alitoa rai kwa wazazi kutoepuka majukumu yao ya kutafuta na badala yake kuwatwisha mizigo watoto na kuwataka kuzingatia misingi ya sheria za kifungu namba 78 kinachokataza utumikishwaji wa watoto walio chini ya umri wa miaka 14 au 18 kwamba wasiendelee kutumikishwa.



## Zanzibar yafanikiwa kutokomeza trakoma

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

ZANZIBAR imefanikiwa kuutokomeza ugonjwa wa vikope (trakoma) ambapo kwa sasa sio tishio tena kwa afya za wananchi wa kisiwa hicho.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi wa Mpango wa Kimataifa wa kupambana na maradhi ya vikope kutoka Shirika la Afya Duniani (WHO), Paul Emerson, wakati akiwasilisha taarifa ya ugonjwa huo kwa viongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wa Wizara ya Afya.

Dk. Emerson alisema dunia inajivunia mafanikio makubwa yaliyofikiwa Zanzibar katika kupambana na maradhi hayo ambapo awali yalikuwa tishio kwa afya za wananchi na hadi sasa yametokomezwa.

Alisema mafanikio hayo yanatakiwa kuigwa na baadhi ya nchi za bara la Afrika na dunia kwa ujumla ili wananchi wake kuwa salama na tishio la maradhi hayo.

''Dunia inashuhudia mafanikio makubwa yaliyofikiwa na Zanzibar katika kukabiliana na kutokomeza maradhi ya vikope kutoka asilimia 11.4 katika mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 1.2 katika mwaka 2023,'' alisema.

Akizungumza katika mkutano huo wa kupokea taarifa hiyo, Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, alisema mafanikio hayo yamefikiwa kutokana na ushirikiano mzuri wa wadau wa maendeleo pamoja na wizara yenyewe na wananchi kutokomeza ugonjwa huo.

Alisema kupitia ushirikiano huo, wamefanikiwa kutokomeza ugonjwa huo katika Wilaya ya Micheweni Pemba ambayo ilikuwa ikiongoza kuwa na wagonjwa wengi.

''Tunashukuru sana Zanzibar tumeyafikia malengo yaliyowekwa na taasisi za kimataifa ifikapo mwaka 2023 kuona kwamba ugonjwa huo unatokomezwa moja kwa moja ambapo tumefikia kiwango cha asilimia 12,'' alisema.

Naye Mratibu wa Huduma za Macho wa Wizara hiyo, Dk. Fatma Juma Omar, alisema jitihada mbalimbali zimechukuliwa katika kukabiliana na ugonjwa huo ikiwamo upatikanaji wa dawa na vifaa tiba.

Alisema kazi iliyopo kwa sasa ni kushajihisha wananchi kujikinga na maradhi hayo ikiwamo matumizi sahihi ya vyoo, utumiaji wa majisafi na salama na kuwapatia wanafunzi elimu shuleni ya kujikinga na ugonjwa huo ambao uliathiri zaidi maeneo ya Wilaya ya Micheweni Pemba.

# Kasi mfumuko wa bei yashuka Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KASI ya kiwango cha mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia Oktoba 2023, imeshuka hadi asilimia 6.50 kutoka asilimia 7.45 iliyosajiliwa Septemba mwaka huu.

Hayo yameelezwa juzi na Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Hassan Jamal Hassan, alipokuwa akiwasilisha ripoti ya mfumuko wa bei kwa mwezi Oktoba, Mazizini, Zanzibar.

Alisema, kushuka kwa kiwango cha mfumuko kulichangiwa zaidi na kushuka kwa bei za bidhaa za vyakula na vinywaji visivyo na vileo kwa asilimia 11.4 Oktoba 2023 ikilinganishwa na asilimia 13.94 mwezi Septemba.

Aidha, alisema, faharisi za bei zimeongezeka kufikia 107.25 mwezi Oktoba 2023 ukilinganisha 100.71 Oktoba mwaka 2022.

Alizitaja bidhaa zilizopelekea kushuka huko ni pamoja na mafuta ya kupikia (25.2%), ndizi za mkono mmoja (10.2%), ndizi mtwike (4.3%), muhogo (11.0%), majimbi (3.4%) na viazi vitamu (1.2%).

Meneja Msaidizi Idara ya Uchumi Benki Kuu Tawi la Zanzibar, Moto Ng'winganele Lugobi, alisema, kupungua kwa kasi ya mfumuko wa bei ni hatua nzuri ya kiuchumi na malengo yaliokuwapo ya kubakia kwenye tarakimu moja.

"Ni ahueni kwa wananchi na hii inatokana na kuwapo kwa bidhaa za kutosha kwenye masoko. Lakini kwa ujumla hali ya uchumi imeendelea kubakia vizuri na hata upatikanaji wa dola hivi sasa upo vizuri,"alisema.

Alisema mfumuko wa bei kwa kipimo cha mwaka unapima kiwango cha kasi ya mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma zote zinazotumiwa na kaya binafsi.

Alisema bidhaa zitakapokuwa bei ya juu itakuwa mzigo kwa mtumiaji, lakini, zikishuka sana mzalishaji atashindwa kuendelea na uzalishaji.

Hata hivyo, alisema, bado hali ya kiuchumi inabakia vizuri kutokana na kuwapo kwenye tarakimu moja ambayo ndiyo njia bora ya kuwavutia wawekezaji kwa ajili ya kuwekeza nchini.

Mchumi Mkufunzi Mwandamizi wa Shule ya Biashara, Dk. Estella Ngoma Hassan, alisema, kushuka huko kwa kiwango cha mfumuko ni hali ya kawaida kulingana na mwenendo wa kibiashara.

Alisema, pamoja na kupanda kidogo kwa mfumuko, hali ya uchumi imeendelea kubakia vizuri huku kukiwa na bidhaa za kutosha kwenye masoko na uzalishaji mzuri.

Aidha, alisema, kuwapo kwenye tarakimu moja, ni njia bora ya kuwavutia wafanyabiashara kuwekeza nchini kwa ajili ya maendeleo ya taifa.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (kulia) na Makamu wa Rais Mtendaji wa Benki ya Afrexim, Kanayo Awami, wakibadilishana mkataba wa makubaliano ya dola milioni 115 baada ya kutiliana saini, nchini Misri jana, ili kuimarisha uwekezaji katika sekta muhimu za kilimo, mafuta, gesi na biashara nchini Tanzania na Burundi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ZAFELA yasisitiza ushiriki wa jamii kutokomeza udhalilishaji wanawake

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JUMUIYA ya Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA) imesema jamii inawajibu wa kushirikiana na wanaharakati katika kukomesha vitendo vya udhalilishaji kwa wanawake na watoto kwa sababu ni janga kubwa kitaifa.

Hayo yalisemwa jana visiwani humo na mratibu wa mradi wa upatikanaji wa haki kwa wanawake na watoto kutoka ZAFELA, Mwanaisha Mustafa, wakati akiongoza majadiliano ya wanadawati na walimu wa shule kuhusu uundaji wa madawati ya wanafunzi wa shuleni katika kupinga udhalilisha kwa watoto.

Alisema licha ya wanaharakati kuchukuwa nafasi kubwa ya kupinga lakini bado matendo hayo yanaendelea hivyo kuwepo kwa madawati ya wanafunzi kutasaidia kukomesha vitendo hivyo.

Alisema ZAFELA imeona ipo haja kuja na mpango huo ili kuwajengea uwezo wanafunzi wadogo kufahamu matendo hayo wanapofanyiwa na kuyaripoti ili kuchukuliwa hatua stahiki.

Aidha alisema vitendo hivyo vinawarudisha nyuma watoto wadogo ambao ni wanafunzi hivyo wakati umefika kwa walimu na wakuu wa madawati kushirikiana katika kuanzisha madawati ya wanafunzi shuleni.

Alisema wanafunzi wengi wanapofanyiwa matendo hayo huwaumiza kisaikolojia na kushindwa kuendelea na masomo yao, hivyo niwajibu wa walimu kuwa sasa kushirikiana na wanafunzi pale madawati hayo yatakapo kamilika.

Mratibu huyo alisema ZAFELA inatekeleza mradi wa kupinga vitendo vya udhalilishaji chini ya ufadhili wa Shirika la Kimataifa la UNDP ili kurahisisha upatikanaji wa haki kwa watoto na wanawake na kuwa salama wakati wowote.

Alisema ZAFELA itafanya ushawishi mkubwa madawati hayo yanasimama ili wanafunzi waliyofanyiwa vitendo hivyo wawe na ujasiri wa kuripoti na kuelimishwa wasifanyiwe tena vitendo hivyo.

Wakichangia katika mjadala washiriki wakiwamo walimu walisema hivi sasa wanafunzi wa shule hawako salama na kuna baadhi ya shule wanafunzi wakijihusisha na utumiaji wa mihadarati.

Mwalimu wa Shule ya Msingi Kiembe Samaki, Zakia Salim, aliwataka wazazi na walezi kufuatilia mienendo ya watoto wao ili kujua mabadiliko yao ya kimwili na kiakili hali ambayo itasaidia kuwakinga na vitendo vya udhalilishaji.

Aidha, alishauri kufanyiwa marekebisho sheria ya mtoto ili kupunguza wimbi la watoto kudhalilishana kwa sababu sheria ya mtoto Zanzibar ya mwaka 2011 haimtii hatiani mtoto anayefanya makosa hayo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**MOZA YAHAYA SULTAN** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1009/0058** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia BABATI DAY SEKONDARI mwaka 2009. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MTW/MTW/RB/343297/2022.**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**DEO FREDI KINDOLE** anatangaza kupotelewa kwa hati ya kusafiria namba **TAE131518** iliyotolewa makao makuu. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/RUV/TUN/628/2023**

**JAMHURI YA MUUNGANOI WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya MKURANGA**

**Kituo cha MKURANGA, Mkoa PWANI**

**Shauri la Ndoa Na 64/2023**

**Jina la mdai..........................................ZENA ISSA IMRAN**

**Jina la Mdaiwa...............................SAIDI RASHIDI KHATAU**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa SAIDI RASHIDI KHATAU**

**Popote ulipo**

**Kwa kuwa mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba (Eleza hapa habari za Madai)**

Mdai amefungua shauri dhidi yako la talaka na mgawanyo wa mali kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 22 mwezi 11 mwaka 2023 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 13 mwezi 11 mwaka 2023

HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO MKURANGA

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NDUGU ANNA EVARIST MYOVELLA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T161 DPD** aina ya **TOYOTA IST.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi namba **PHQ/DOD/DOD/RB/8849/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**RAMADHAN HUSSEIN GIRO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 580 AJN.** Chassis namba **16516665** na Engine namba **212JA43883.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/ARU/ARU/6617/2023.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA KINGOLWIRA**

**KITUO CHA ............. MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na......5/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: ISA AMRI wa kingolwira**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA YAHAYA KAMBI**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 29 Mwezi 11 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia.

Imetolewa leo tarehe 7 mwezi 11 mwaka 2023

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI......478......... LA 2023**

**ANETH N. PAULO..................MUOMBAJI/WAOMBAJI**

**DHIDI YA**

**PATRICK LUCIANO MBEDULE.........MDAIWA/WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**

**PATRICK LUCIANO MBEDULE**
**POPOTE ULIPO/MLIPO:**

**ANETH .N. PAULO** Amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni (Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa tarehe 27/11/2023 saa 03:00 Asubuhi/mchana mbele ya Mh J.W SILLAS Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

Imetolewa na kutiwa saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 26 Mwezi ..10..,2023

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA MWANZO IRINGA MJINI**

**SHAURI LA TALAKA NO.46/2023**

**YUNISI SHABANI NDOMONDO..........MADAI**

**v/s**

**PROSPER KALIST MASSAO..........MDAIWA**

Unatakiwa kufika Mahakamani tarehe 30/11/2023 saa2:30 asubuhi kwa jili ya shauri la talaka usipofika shauri litasikilizwa upande mmoja na kutolewa maamuzi.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 15/11/2023.

**TANGAZO HILI LITOKE KESHO TAREHE 16/11/2023**

HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO IRINGA MJINI.

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**


**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0745 700 710.

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

**HABARI KIMATAIFA**

# Mvutano waongezeka baada ya hospitali kuvamiwa Gaza

- Hamas: Huo ni uhalifu dhidi ya binadamu
- Canada yaisisitiza Israel kuacha kuua watoto

**Na Maulid Mmbaga**

OFISI ya habari ya serikali ya Hamas imesema uvamizi wa Jeshi la Israel katika hospitali ya Al-Shifa ya Gaza ni uhalifu dhidi ya binadamu, kivita na kimaadili.

Jeshi la Israel lilivamia na kuizingira hospitali ya Al-Shifa huko Gaza jana kwa madai kwamba Hamas wanaendesha shughuli na mipango ya kijeshi kwenye mahandaki yanayodaiwa kuwepo chini ya hospitali hiyo, madai ambayo Hamas inayakanusha.

Kwa mujibu wa Hamas wagonjwa 9,000, wahudumu wa afya na raia walioyakimbia makazi yao walikuwa hospitalini hapo wakati uvamizi huo ulipofanyika usiku.

Katika video iliyosambazwa kupitia mtandao wa X, (zamani Twitter,) na Kituo cha Habari cha Palestina, kiongozi wa Hamas Izzat al-Rishq, anasema Israeli ilishambulia kituo cha kiraia, na sio eneo la kijeshi.

Katika taarifa ya awali, kundi la Hamas ambalo limepigwa marufuku nchini Marekani, Uingereza na Umoja wa Ulaya (EU), inasema inaiwajibisha Washington na Rais wa Marekani Joe Biden kuhusika na uvamizi huo.



Wagonjwa na raia wakiwa ndani ya Hopitali ya Al-Shifa huko Gaza. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**MAREKANI**

Licha ya madai hayo Ikulu ya Marekani inadai kuwa wanamgambo wa Kipalestina wana kituo cha udhibiti katika hospitali ya Al-Shifa huko Gaza, kauli inayounga mkono utetezi wa Israeli wa harakati za kijeshi kwenye kituo hicho.

Msemaji wa mshauri wa usalama wa taifa wa Marekani John Kirby akinukuu vyanzo vya kijasusi vya Marekani, anasema Hamas na kundi la wanamgambo la Islamic Jihad la Palestina, wanaendesha kituo na kudhibiti mtandao mpana kutoka hospitali ya Al-Shifa huko Gaza City.

"Tunazo taarifa kwamba Hamas na kundi la Islamic Jihad la Palestina walitumia baadhi ya hospitali katika Ukanda wa Gaza, ikiwa ni pamoja na hospitali ya Al-Shifa na mahandaki ya chini kuficha na kusaidia operesheni zake za kijeshi na kuwashikilia mateka.

"Hamas na wanachama wa Islamic Jihad wanaendesha kamandi na kudhibiti mtandao huo kutoka Al-Shifa katika Jiji la Gaza. Wamehifadhi silaha huko na wako tayari kujibu operesheni ya jeshi la Israeli dhidi ya hospitali hiyo," amesema.

Kauli hiyo ya Marekani, inayoungwa mkono na Wizara ya Mambo ya Nje na ya ulinzi ya Pentagon, inatolewa wakati shinikizo likiongezeka kwa Israel kutokana na kuizingira hospitali kubwa ya Al-Shifa, ambapo madaktari wanasema wagonjwa na watu wanaotafuta makazi wamekwama katika mazingira ya kutisha.

Hamas inasema matamshi hayo ya Ikulu ya White House yanachochea mauaji zaidi katika hospitali za Gaza.

**UN**

Umoja wa Mataifa (UN) unakadiria kwamba takribani watu 2,300, wakiwemo wagonjwa, wafanyakazi na raia waliohamishwa, wamekwama ndani ya kituo hicho na watashindwa kuondoka kutokana na mapigano makali yanayoendelea karibu na kituo hicho.

> **"Hamas na wanachama wa Islamic Jihad wanaendesha kamandi na kudhibiti mtandao huo kutoka Al-Shifa katika Jiji la Gaza.**

Aidha, licha ya wito wa kusitisha mapigano, jeshi la Israel limedai kudhibiti jengo la bunge la Gaza na taasisi nyingine za serikali zinazoendeshwa na kundi la Hamas katika eneo hilo, wakati wanajeshi wake wakizidisha mashambulizi kwenye maeneo ya Wapalestina.

Taarifa hiyo inaongezea kwamba taasisi za serikali za shirika la kigaidi la Hamas zimetumika kwa malengo ya kijeshi ikiwa ni pamoja na mafunzo ya kujiandaa kwa shambulio dhidi ya Israeli Oktoba saba, mwaka huu.

Hata hivyo Hamas imepuuzia taarifa za jeshi la Israel za udhibiti wa taasisi zake. Huku ofisa mmoja mwandamizi ndani ya Hamas Bassem Naim, akisema kwamba hatua hiyo ilikuwa ni jaribio la kusikitisha na la kutengeneza ushindi na udhibiti wa kifikra wa maeneo matupu au ambayo yalilengwa na kuharibiwa awali.

Kando na yanayoendelea ndani ya Gaza, juhudi za kidiplomasia za kutatua mzozo huo nazo zinatajwa kuendelea na kwamba Qatar imetoa wito kwa Israel na Hamas kufikia makubaliano ya kuwaachia mateka, ikionya kwamba hali inayoendelea Gaza inazidi kuwa mbaya kila kukicha.

Akizungumza na vyombo vya habari mjini Doha, msemaji katika wizara ya mambo ya nje ya Qatar, Majed bin Mohammed Al-Ansari anasema hali ya kuzorota huko Gaza inatatiza juhudi za upatanishi.

Vilevile, anaeleza kuwa wanaamini hakuna nafasi nyingine kwa pande zote mbili zaidi ya upatanishi huo kufanyika na kufikia hali ambayo italeta mwanga wa matumaini katika mgogoro huo mbaya.



Kiongozi wa Hamas, Khaled Meshaal.

Pia inaelezwa kuwa taifa hilo la Ghuba limeongoza mazungumzo ya kuachiliwa kwa mateka na usitishaji mapigano kwa muda sasa.

Siku chache zilizopita kundi la Hamas lilisema Israel imeomba kuachiliwa huru kwa wanawake 100 na watoto kwa mabadilishano ya watoto 200 wa Kipalestina na wanawake 75 wanaoshikiliwa katika jela za Israel.

**CANADA**

Naye, Waziri Mkuu wa Canada Justin Trudeau, anatoa wito kwa Israel kuacha kuua watoto, jambo lililosababisha kupata majibu ya tofauti kutoka kwa mwenzake wa Israel Benjamin Netanyahu.

Trudeau anasema kwamba mauaji ya wanawake, watoto na watoto wachanga katika Ukanda wa Gaza uliozingirwa lazima yakomeshwe, akisisitiza kuwa Hamas inawajibika kwa vifo vya raia huku vikosi vya Israel vikiendelea kushambulia eneo hilo.

"Ninaiomba serikali ya Israel kujizuia zaidi," amesema Trudeau katika ukosoaji wake mkali kwa Israeli tangu vita dhidi ya Gaza kuzuka zaidi ya wiki tano zilizopita.

"Ulimwengu unatazama, kwenye TV, kwenye mitandao ya kijamii tunasikia ushuhuda wa madaktari, wanafamilia, walionusurika, na watoto ambao wamepoteza wazazi wao, ulimwengu unashuhudia mauaji haya ya wanawake, watoto na watoto wachanga, hili lazima

Waziri wa Ulinzi wa Israel Netanyahu, alimjibu waziri huyo wa Canada akisema "Sio Israeli ambayo inalenga raia kimakusudi bali ni Hamas ambayo ilikata vichwa, kuwachoma na kuwaua raia katika hali ya kutisha zaidi kuwahi kutekelezwa kwa Wayahudi tangu mauaji ya Holocaust."

"Majeshi ya ustaarabu lazima yaunge mkono Israeli katika kuushinda ukatili wa Hamas," amesema Netanyahu.

Licha ya hayo, Canada inaeleza kuwa Israel ina haki ya kujilinda dhidi ya Hamas baada ya kundi la Wapalestina kushambulia eneo la kusini mwa Israel Oktoba saba na kuua watu 1,200.

Lakini pia inaeleza wasiwasi wake juu ya kuongezeka kwa idadi ya vifo katika eneo lililopigwa na kuzingirwa, ambako zaidi ya Wapalestina 11,200 wanadaiwa kuuawa na Israeli tangu mzozo huo uanze.

***Chanzo mashirika ya kimataifa***

# KATWILA APIGIA HESABU POINTI 12 KWA MECHI 4

Na Saada Akida

KOCHA Mkuu wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila ameanza kupigia hesabu pointi 12 katika michezo minne ya ugenini inayofuata ya Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo ni sawa na dakika 360.

Mtibwa Sugar watakuwa ugenini wakianza dhidi ya Azam FC mchezo utakaopigwa Novemba 24 na baada ya hapo itafunga safari kuwafuata Tabora United Desemba mosi.

Wakimalizana na Tabora United watasafiri kwenda Mkoani Lindi kucheza na Namungo kwenye uwanja wa Majaliwa, Ruangwa Desemba 7 na sijku tatu baadae watakuwa na kibarua cha kuwakabili Yanga kwenye uwanja wa Azam Complex, Chamazi.

Akizungumza na Nipashe jana, Katwila alisema malengo yao ni kutafuta alama tatu kila mechi ili kujiondoka katika nafasi ya mwisho kwenye msimamo wa ligi hiyo ambayo wapo sasa.

Alisema anafahamu michezo hiyo haitakuwa rahisi lakini wamejipanga kuhakikisha wanavuna alama ili kujiondoa katika nafasi mbaya waliyopo sasa kwenye msimamo wa Ligi Kuu.

"Ligi ni ngumu na ukizingatia tumecheza michezo tisa na hatujafanya vizuri, tumeona madhaifu yetu na kwa sasa tuko uwanja wa mazoezi kujiandaa vizuri na kufanyia kazi mapungufu yetu ili tukienda kwenye mechi tusirudie makosa ambayo yalitugarimu awali.

"Mikakati yetu kwa sasa ni kushinda na kutafuta pointi katika hizo mechi ili kuweza kukusanya alama tatu au moja, kwa sababu hakuna mechi rahisi unapojiandaa na mpinzani wako naye anajiandaa," alisema Katwila.

Mtibwa Sugar ipo mkiani katika msimamo wa ligi ikiwa imekusanya alama tano tu katika michezo tisa ambayo imechezwa mpaka sasa wakishinda mchezo mmoja, sare mbili na kufungwa michezo sita.





Baadhi ya wachezaji wa klabu ya Simba Queens wakiwa kwenye mazoezi ya timu hiyo jijini Dar es Salaam jana. PICHA: MPIGA PICHA WETU

# Mdoe amuweka kando Mpenda Australia

Na Saada Akida

KAMPUNI ya promosheni ya ngumi za kulipwa nchini Australia na waandaaji wa pambano la ubingwa wa WBC Peace lililokuwa limkutanishe Mtanzania Pius Mpenda na Joel Camilleri wa nchini humo, imemuondoa Mpenda kucheza pambano hilo baada ya kukiuka makubaliano.

Nafasi ya Mpenda katika pambano hilo amepewa Mtanzania mwingine Nicolaus Mdoe atakayepanda ulingoni Desemba 16 kupambana na Camilleri katika ukumbi wa The Melbone, Flemington Victoria nchini humo.

Camilleri mwenye rekodi ya kucheza mapambano 35 akiwa ameshinda 26 kati ya hayo 13 ni kwa KO huku akipigwa kwenye mapambano nane na kutoka sare moja huku Mdoe akiwa na rekodi ya kucheza mapambano 21, ameshinda 13 kati ya hayo tisa ni kwa KO na amepoteza mapambano sita kati ya hayo matatu ni kwa KO huku akitoka sare mara mbili.

Akizungumza na Nipashe jana, Wakala wa pambano hilo kutoka hapa Tanzania, Emmanuel Mlundwa, alisema wamelazimika kumuondoa Mpenda katika pambano hilo kutokana na kuharibu makubaliano ya mkataba wake ambayo yalimtaka asipigane kwa siku 45 baada ya kusaini mkataba lakini badala yake bondia huyo aliendа kupigana Uturuki kinyume na makubaliano ya mkataba wake.

"Mpenda hatoweza kwenda tena Australia kwa sababu ya matatizo ya kuharibu mkataba wake hivyo wameamua kumchukua Nicolas Mdoe na maandalizi ya safari yameanza haraka.

"Kilichotokea ni Mdoe kuvuruga makubaliano ya mkataba sasa wale jamaa wemekuwa na hofu ya anaweza akuvuruga tena kwa makusudi ndiyo maana wameona wamuondoe mapema, " alisema Mlundwa.

Aliongeza kuwa bado kuna shida kubwa kwa mabondia wa Tanzania katika kuheshimu mikataba hali inayopelekea kutokuaminika kwa makampuni ya ngumi mbalimbali ndani na nje ya nchini.

## Dk Tulia: Bunge Marathon kukusanya fedha

Na Gwamaka Alipipi, aliyekuwa DODOMA

SPIKA wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk Tulia Ackson amesema kuwa mashindano ya riadha ya Bunge Marathon yatakayoanza Aprili 13 mwakani yatachangisha fedha na mali kwa lengo maalum litakalokuwa likipangwa kabla ya mashindano hayo.

Hivi Karibuni Bunge limezindua mashindano hayo ya marathon jijini Dodoma yatakayokuwa yakihusisha wabunge na wananchi.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mashindano hayo, Dk.Tulia alisema mashindano hayo yatakuwa yakifanyika kila mwaka na yatakuwa na malengo mahususi ya kuchangisha rasilimali fedha na mali kwa lengo maalum litakalokuwa likipangwa kila mwaka.

"Mbio Maalumu zitakazojumuisha washiriki kutoka katika makundi mbalimbali ya jamii yetu, katika mazingira rafiki nje ya Ofisi, bila kujali wadhifa, jinsi au umri wa mshiriki, na hivyo kuleta kufahamiana zaidi, kufurahia michezo kwa pamoja na hatimaye kujenga umoja miongoni mwetu." alisema na kuongeza, "

"Pia yatatoa fursa kwa wananchi kushiriki pamoja na Wawakilishi wao waliopo Bungeni, Watumishi wa Ofisi ya Bunge, wadau mbalimbali, wanamichezo wa makundi mbalimbali katika mbio hizo zitakazokuwa za wazi kwa yeyote atakayependa kushiriki kutoka ndani au hata nje ya nchi,"alisema

Aidha, Dk Tulia alisema michezo hiyo pia itatumika na Bunge kujiandaa kwa ajili ya kushiriki mashindano mbalimbali ikiwemo michuano ya Mabunge ya Afrika Mashariki (EALA Games) kupitia Timu ya Bunge Sports Club na michuano ya SHIMIWI kwa upande wa Watumishi pekee.

Alisema mbali na mashindano ya riadha, Bunge pia linaendesha Bunge Bonanza ambalo linawakutanisha Wabunge na Watumishi kwa ajili yakufanya mazoezi na kuweka utimamu wa mwili na kujenga afya njema.

Hii si mara ya kwanza kwa bunge kuchangisha fedha kupitia wabunge na wadau mbalimbali kwa ajili ya kushiriki maendeleo ya jamii ambapo imeweza kujenga shule ya sekondari ya wasichana ya mchepuo wa sayansi.

Pia, Bunge lilishiriki kampeni kubwa ya kutatua upungufu wa madawati kwa kuchangia Sh bilioni 6 zilizotengeneza madawati katika shule za umma.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### UNITED KUMUUZA CASEMIRO

KLABU ya Manchester United itaangalia uwezekano wa ofa kwa kiungo wa kati wa Brazil Casemiro, huku timu za Ligi Kuu Saudia zikilenga kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 kwa fedha nyingi. ***(Talksport)***

### CHELSEA YAMKANA OSIMHEN

KLABU ya Chelsea haina nia na uwezekano wa kumnunua mshambuliaji wa Napoli na Nigeria, Victor Osimhen mwenye umri wa miaka 24 katika dirisha la uhamisho la Januari. ***(Football London)***

### TADIBO KUTUA UNITED

KIUNGO wa kati wa Nice na Ufaransa, Jean-Clair Todibo mwenye umri wa miaka 23, ameibuka kama mtu anayelengwa sana na Manchester United Januari. ***(Mail)***

### UNITED, SPURS VITANI

MANCHESTER United na Tottenham Hotspur zimeungana na Liverpool na Arsenal katika mbio za kumsajili kiungo wa kati wa Fluminense na Brazil, Andre mwenye umri wa miaka 22. ***(90minutes)***

### RAPHINHA SOKONI RASMI

BARCELONA imeweka ada ya uhamisho ya mshambuliaji wa Brazil, Raphinha mwenye umri wa miaka 26 kuwa euro milioni 70. ***(Football Transfers)***

### FORSBERG KWENDA MAREKANI

KIUNGO wa kati wa Sweden, Emil Forsberg, 32, amekubali kwa maneno yake kujiunga na New York Red Bulls kutoka RB Leipzig ifikapo Januari. ***(Fabrizio Romano)***

### NEVES ANUKIA ARSENAL

ARSENAL imearifiwa kuhusu uwezekano wa kupatikana kwa kiungo wa kati wa Al-Hilal na Timu ya Taifa ya Ureno, Ruben Neves, 26, wakati wa dirisha la Januari. ***(90min)***

### PALHINHA ATOA NENO

KIUNGO wa kati wa Fulham na Ureno, Joao Palhinha, 28, amesema uhamisho wake wa siku ya mwisho ya kufungwa kwa dirisha la usajili ambao haukufanikiwa wa kwenda Bayern Munich "uliniathiri sana". ***(Mail)***

### JUVE YAMTAKA SANCHO

JUVENTUS iliwasiliana na Manchester United kuhusu mkataba wa mkopo wa winga wa Timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho, 23, wiki iliyopita. ***(Mail)***

### JORGINHO KUREJEA ITALIA

KIUNGO wa kati wa Arsenal, Jorginho mwenye umri wa miaka 31 amesema angependa kurejea nyumbani na kuchezea klabu ya Italia kabla ya mwisho wa soka yake. ***(Metro)***

### MABAO KUMTAJIRISHA KANE

MSHAMBULIAJI wa Bayern Munich na England, Harry Kane, 30, ana kipengele katika mkataba wake kinachosema endapo atafunga zaidi ya mabao 40 katika michuano yote kwa msimu mmoja, atapokea euro 250,000. ***(Sport Bild via Christian Falk)***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# NEYMAR KUKOSEKANA DIMBANI MUDA MREFU

**SAO PAULO,** Brazil

### ●●● Ni kutokana na kufanyiwa upasuaji wa goti ambao...

NEYMAR anakabiliwa na kukaa nje muda mrefu kutokana na jeraha lake baya la goti, kwa mujibu wa daktari wa timu ya taifa ya Brazil, Rodrigo Lasmar.

**Fowadi huyo wa Al Hilal alifanyiwa upasuaji wa kurekebisha goti lake la kushoto Novemba 2, mwaka huu nchini Brazil.**

Hakuna makadirio ya kupona yaliyotolewa, lakini Shirikisho la Soka la Brazil (CBF), linatumaini Neymar mwenye umri wa miaka 31 atarejea kwa wakati kwa ajili ya mashindano ya Copa America 2024, ambayo yatafanyika Marekani kati ya Juni 20 na Julai 14, mwakani.

"Neymar amekuwa akipata nafuu sana," alisema Lasmar, ambaye alimfanyia upasuaji mchezaji huyo.

"Nilikuwa na mchezaji huyo kwa ajili ya tathmini mpya ya baada ya upasuaji, iliyopangwa tayari. Anaendelea vizuri sana, bila shaka, bado katika awamu ya kwanza.

"Ni jeraha tata, alipasuka goti na anahitaji kuwa nje ya uwanja kwa muda mrefu kutokana na majeraha yanayohusiana, atapitia mchakato mrefu wa ukarabati wa goti, anafahamu hilo. Lakini amekuwa akijibu vizuri sana, tumeridhika."

Neymar, ambaye alijiunga na klabu ya Ligi Kuu ya Saudi Aarabia, Al Hilal majira ya joto kwa uhamisho wa euro milioni 90 kutoka PSG, aliumia wakati Brazil ilipofungwa na Uruguay kwenye mchezo wa kufuzu kwa Kombe la Dunia Oktoba.

Mfungaji bora wa muda wote wa Brazil kwa wanaume, amekabiliwa na majeraha ya muda mrefu.

Nyota huyo wa zamani wa Barcelona amepata majeraha kadhaa ya kifundo cha mguu wa kulia na mguu siku za nyuma, ambayo yalimlazimu kukosa kucheza kwa wiki sita mwaka 2021 na kampeni ya ushindi ya Brazil ya Copa America 2019.

Majeraha yamemzuia Neymar kufikia mechi 17 pekee kwa klabu na nchi mwaka huu. Februari akiwa na Paris Saint-Germain alijeruhiwa kifundo cha mguu na kukaa nje ya uwanja kwa miezi mitano.

"Ni muhimu sana kuelewa jeraha baya alilopata," alisema Lasmar.

"Amekuwa na majeraha na hali zingine hapo awali, hii ilikuwa upasuaji wake wa tatu. Nilishiriki katika zingine mbili, zilikuwa na vipindi vifupi. Wakati huu ni jeraha kubwa zaidi, inachukua muda zaidi, kwa hivyo tunahitaji kuwa mwangalifu sana, amejitolea kupona. Anafuata kila kitu tunachopendekeza."

Pia Lasmar aliwahakikishia mashabiki wa Arsenal kwamba, Gabriel Jesus hataharakishwa kurejea kutokana na jeraha lake la paja.

Fowadi huyo wa Arsenal alijumuishwa katika kikosi cha Brazil kwa ajili ya mechi zijazo za kufuzu kwa Kombe la Dunia dhidi ya Colombia utakaopigwa leo na mwingine dhidi ya Argentina utakaochezwa Novemba 21, mwaka huu.

HABARI MICHEZO

# UNITED YAJIANDAA KUMKOSA ONANA




**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United wamejipanga kumkosa, André Onana wakati wa michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2023), Januari ingawa golikipa huyo bado hajafanya uamuzi kama ataicheza Cameroon, vyanzo vimeiambia ESPN.

Kocha wa United, Erik ten Hag, anapanga kutomkosa Onana kwa muda wote wa michuano hiyo, itakayoanza Januari 13 hadi Februari 11, mwakani huko Ivory Coast.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 anaweza kukosa mechi nne za Ligi Kuu England kama Cameroon itatinga fainali itakayochezwa Februari 11, mwakani.

Ten Hag hajafahamishwa rasmi lakini Mholanzi huyo, kulingana na chanzo, anaelewa hali hiyo na atamruhusu Onana kufanya uamuzi wake kuhusu kushiriki au kutoshiriki.

United waliambiwa wakati wa mazungumzo ya kumsajili Onana kutoka Inter katika majira ya joto alikuwa amestaafu soka la kimataifa baada ya kuondoka mapema kwenye Kombe la Dunia kule Qatar.

Tangu wakati huo aliitwa kikosini kusaidia Cameroon kufuzu kwa AFCON na amechaguliwa kwa mechi za kufuzu kwa Kombe la Dunia 2026 dhidi ya Libya na Mauritius wakati wa mapumziko ya Novemba hii.

Chanzo kimoja kimeiambia ESPN Onana atafanya uamuzi wa mwisho kuhusu kusafiri na kikosi kuelekea Ivory Coast karibu na wakati na baada ya mazungumzo na Shirikisho la Soka la Cameroon.

United wanaamini wako tayari kwa uwezekano wa kuondoka kwa Onana baada ya kumsajili mchezaji wa kimataifa wa Uturuki, Altay Bayindir kutoka Fenerbahce majira ya joto.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 bado hajacheza mechi yake ya kwanza pale United lakini vyanzo vimeiambia ESPN tayari amewavutia katika mazoezi.

Kumpoteza chaguo la kwanza la Onana bado kunaweza kumfadhaisha Ten Hag, ambaye tayari anakabiliana na orodha ya majeruhi inayoongezeka.

Christian Eriksen na Rasmus Højlund ndio wachezaji wa hivi karibuni ambao wamepata matatizo na kujiunga na Lisandro Martínez, Casemiro, Luke Shaw, Tyrell Malacia na Jonny Evans wakiwa nje ya uwanja.



# Mazzarri amrithi García Napoli

**NAPLES,** Italia

NAPOLI imemwajiri, Walter Mazzarri kama kocha wao mkuu baada ya kumtimua, Rudi García miezi minne tu ya uongozi wake, klabu hiyo ilitangaza jana.

Mazzarri, ambaye aliwahi kuwa kocha wa mabingwa hao wa Italia kuanzia 2009 hadi 2013, ameripotiwa kusaini mkataba wa hadi mwisho wa msimu huu.

Klabu hiyo alitangaza hatua hiyo katika chapisho kwenye mtandao wa X zamani Twitter, ikisema "Karibu tena Walter!". Baadaye ilithibitisha habari hizo kwenye chaneli zake za kijamii.

Kuajiriwa kwake kunafikisha mwisho wa enzi ya García iliyodumu kwa muda mfupi, huku Napoli ikiona kichapo cha bao 1-0 nyumbani dhidi ya Empoli kikiwa cha mwisho.

"SSC Napoli imefanya uamuzi wa kumwondoa mara moja kocha wa kikosi cha kwanza Rudi Garcia," ilisema taarifa ya klabu hiyo.

"Klabu ingependa kumshukuru Rudi na wakufunzi wake kwa bidii yao."

Napoli inashika nafasi ya nne katika msimamo wa Serie A ikiwa na pointi 10 nyuma ya viongozi wa, Inter Milan.

Kiwango cha nyumbani kilimtatiza sana García, na ushindi wa mwisho wa timu katika mashindano yote kwenye Uwanja wa Diego Armando Maradona ukitokea dhidi ya Udinese mnamo Septemba 27, mwaka huu. Garcia mwenye umri wa miaka 59, raia wa Ufaransa alikuwa na mafanikio ya kutosha akiwa na AS Roma kuanzia mwaka 2013 hadi 2016 wakati wa kazi yake ya awali nchini Italia.

Lakini hakupata matokeo yaliyotarajiwa katika kazi yake ya hivi majuzi zaidi katika klabu ya Al Nassr, timu ya Saudi Arabia ambayo Cristiano Ronaldo alijiunga nayo baada ya Kombe la Dunia.

# Dalot ajiondoa kikosini Ureno

**LISBON,** Ureno

BEKI wa Manchester United, Diogo Dalot amejiondoa kwenye kikosi cha Ureno kwa ajili ya mechi za kimataifa za mwezi huu.

Ureno maarufu kama Selecao tayari wamejihakikishia nafasi ya kushiriki mashindano ya Ulaya msimu ujao baada ya kushinda michezo yao yote nane ya kufuzu hadi sasa na watamaliza Kundi J kwa mechi za ugenini huko Liechtenstein na nyumbani kumenyana na Iceland wiki hii.

Kocha, Roberto Martinez amefanikiwa kuiunda tena Ureno kama kikosi cha kushambulia,- wamefunga mabao 32 katika mechi za kufuzu Euro 2024, 12 zaidi ya timu inayofuata - lakini watalazimika kumaliza mechi zao mbili za mwisho bila huduma hiyo ya Dalot.

United imethibitisha Dalot ameondolewa kwenye kikosi cha kimataifa cha Novemba kutokana na "sababu kibinafsi" na nafasi yake imechukuliwa na beki wa kulia wa Porto, Joao Mario.

Mwakilishi pekee wa Mashetani Wekundu katika maandalizi ya Martinez sasa ni nahodha wa klabu, Bruno Fernandes. Kiwango cha Dalot katika ngazi ya klabu kuelekea dirisha la kimataifa kilishuka.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 ameanza kila mechi kati ya mechi 10 za mwisho za United kwenye Ligi Kuu England, wakati mwingine akicheza kama beki wa kushoto kutokana na majeruhi wengi wa kikosi cha kwanza na kusababisha Erik ten Hag kukosa chaguo.

Licha ya mwanzo mbaya wa msimu huu, Dalot na wachezaji wenzake wa United walicheza mechi mfululizo za Ligu Kuu kwa mara ya kwanza msimu huu kabla ya mapumziko ya kimataifa, wakishinda 1-0 ugenini dhidi ya Fulham na nyumbani kwa Luton.

Mapema wiki hii United ilifichua Christian Eriksen na Rasmus Hojlund pia wamejiondoa kwenye majukumu ya kimataifa.



HABARI MICHEZO

# Kocha Azam akomaa na ubingwa Ligi Kuu Bara

**Na Saada Akida**

KOCHA wa Azam FC, Youssouph Dabo, amesema bado kikosi chake kipo kwenye mbio za ubingwa na kwa sasa wanaendelea na maandalizi kwa ajili ya michezo yao ijayo ya Ligi Kuu.

Alisema katika kipindi hiki ambacho ligi imesimama, wanatarajia kucheza mchezo wa kirafiki dhidi ya Gor Mahia ya Kenya kujiweka vizuri kuelekea kwenye michezo yao ya ligi ku.

Akizungumza na Nipashe jana, Dabo alisema licha ya kupoteza mechi huko nyuma, anaamini ligi ni sawa na riadha za mbio ndefu kwa kuwa bado kuna michezo mingi mbele.

Alisema wanahitaji kujiandaa kama wanavyofanya kwa ajili ya kutafuta matokeo katika michezo iliyopo mbele yao kwa kusaka alama tatu katika kila mechi ili kufikia malengo yao.

"Kwa sasa tunaendelea na mazoezi, tutakuwa na mechi ya kirafiki ya kimataifa ikiwa ni sehemu ya maandalizi yetu na kujiandaa kwa mechi zijazo," alisema Dabo na kuongeza,

"Bado tuna nafasi ya kutwaa ubingwa kwa sababu kuna mechi nyingi mbele yetu, tunapaswa kufanya vizuri kwenye kila mechi bila kuwaangalia wenzetu wanafanya nini, naamini kama tatafanya vizuri kwenye mechi zetu nafasi ya ubingwa bado tunayo" alisema Dabo.

Aidha, alisema anashukuru kwa sasa kwenye kikosi chake hakuna majeruhi na wachezaji wake wamefanya mazoezi kwa muda wa wiki mmoja na mwishoni mwa wiki hii watakuwa na mchezo wa kirafiki wa kimatifa dhidi ya Gor Mahia ya Kenya.

"Mchezo huo utazidi kunipa mwanga wa kuona ubora wa kikosi changu na mapungufu ya kufanyia kazi kabla ya mechi yetu ijayo dhidi ya Mtibwa Sugar," alisema Dabo.

# RAIS MWINYI KUNUNUA KILA BAO KARUME BOYS

**Na Adam Fungamwango**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameahidi kununua kwa Shilingi Milioni moja kila goli litakalofungwa na timu ya taifa ya vijana ya Zanzibar 'Karume Boys' kwenye mchezo wa fainali leo dhidi ya Uganda.

Karume Boys leo inacheza na Uganda kwenye uwanja wa Njeru, Jinja ukiwa mchezo wa fainali wa michuano ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA).

Rais Mwinyi kwenye taarifa yake iliyotolewa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Fatma Hamad Rajab, ameahidi kutoa kiasi hicho cha fedha kwenye kila goli litakalofungwa ikiwa ni hatua ya kuwaunga mkono vijana hao.

Zanzibar itakuwa na kazi moja ya kuwatoa kimasomaso Watanzania na kulipa kisasi kwa timu ya Tanzania Bara baada ya kufungwa na Uganda mabao 2-1 katika mechi ya nusu fainali ya michuano hiyo.

**Kombe hilo litakuwa faraja kwa Watanzania ambao walikuwa na timu mbili kwenye michuano ya Ukanda wa CECAFA.**

Karume Boys ilifanikiwa kutinga hatua hiyo baada ya kuifunga Sudan Kusini kwa mikwaju 4-2 ya penalti, baada ya sare ya bao 1-1 ndani ya dakika 90, huku wapinzani wao wakiondoa Tanzania Bara.

Timu zote ziliongoza kwenye makundi yao, Uganda ikiliongoza Kundi A na Zanzibar Kundi B lililokuwa pamoja na ndugu zao wa Bara waliomaliza wa pili, wakivuka pamoja hatua hiyo na kwenda nusu fainali.

Michuano hiyo inayohitimishwa leo ilianza Novemba 4 nchini Uganda ikizikutanisha timu nane ambapo Kundi A, mbali na Uganda, kulikuwa na timu za Ethiopia, Sudan Kusini na Djibouti, huku Kundi B lilikuwa na Tanzania Bara, Zanzibar, Somalia na Rwanda.



Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo wa Zanzibar, Fatma Hamadi Rajabu akisisitiza jambo wakati akizungumza na waandishi wa Habari Migombani Zanzibar jana kuhusiana na mashindano ya CECAFA yanayomalizika leo nchini Uganda. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Simba SC kumpa rungu kocha kuboresha kikosi

INATOKA UKURASA 24

wataka viongozi na mashabiki wa klabu hiyo kuwa kitu kimoja na kushikamana ili Simba ifanikiwe katika mipango yao hasa kuelekea mchezo wao wa wikiendi hii dhidi ya Asec Mimosas.

"Shukrani kwa mashabiki wetu kuendelea kusapoti timu katika hali yoyote, naomba waendeleze sapoti hiyo na pia nawaomba viongozi tuwe pamoja, tukishirikiana hakuna timu yoyote itakayotufunga hapa nyumbani au kututoa kwenye hatua hii ya makundi au robo fainali," alisema.

Alisema kwa sasa wanatakiwa kusahau kila kitu kilichotokea nyuma katika michezo miwili iliyopita na kuelekeza nguvu na akili katika mechi ijayo dhidi ya Asec Mimosas ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kikosi cha Simba chini ya Kaimu Kocha Mkuu, Daniel Cadena na Selema Matola kwa wachezaji ambao hawako kwenye majukumu ya timu za taifa wanaendelea na mazoezi kujiandaa na mchezo huo utakaochezwa wikiendi ijayo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa Dar es Salaam.

# Nzengeli, Baleke vinara




Nzengeli




Baleke

INATOKA UKURASA 24

eneo la hatari ambao ni Moses Phiri wa Simba, Habib Kyombo wa Singida Fountain Gate ambaye yote ameyafungwa kwa kichwa na kuwa mchezaji anayeongoza kwenye Ligi Kuu kupachika mabao kwa vichwa wakifuatiwa na Prince Dube wa Azam FC, Matheo Antony wa Mtibwa Sugar na Marouf Tchakei wa Singida Fountain Gate.

Michezo
Alhamisi Novemba 16, 2023
Nipashe



Dalot ajiondoa kikosi Ureno UKURASA 22



Golikipa wa Azam FC, Abdulai Iddrisu, akiwa mazoezini katika Uwanja wa Azam Complex juzi. **PICHA: BINZUBEIRY**

# Simba SC kumpa rungu kocha kuboresha kikosi

**Na Saada Akida**

## ●●● Kumkabidhi faili la wachezaji wote atakapowasili ili....

UONGOZI wa klabu ya Simba umesema utamwachia 'rungu' la uamuzi wa maboresho ya kikosi cha timu hiyo kocha mpya wanayetarajia kumtangaza wiki hii.

**Simba imepanga kukiboresha kikosi chake ili kurejesha makali yake na suala hilo litakuwa chini ya kocha huyo mpya.**

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya klabu hiyo, Salim Abdallah 'Try Again', alisema jana kuwa kocha huyo atapewa faili la wachezaji wote na kuangalia mikanda ya mechi zilizopita ili ajiridhishe na uwezo wa wachezaji waliopo.

Alisema kocha ataangalia ni mchezaji gani atamfaa kwenye mipango yake na kutoa mapendekezo kwa uongozi ya nini kifanyike kukiboresha kikosi cha timu hiyo.

Kwa sasa Simba ipo kwenye hatua za mwisho za mchakato wa kutafuta kocha mkuu ambaye atarithi mikoba ya Roberto Oliviera 'Robertinho' aliyetupiwa virago klabuni hapo kufuatia kipigo cha mabao 5-1 kutoka kwa watani zao Yanga.

Baadhi ya makocha wanaotajwa kuwa na uwezekano wa kupewa nafasi ya kurithi mikoba ya Robertinho ni pamoja na Kocha wa USM Alger ya Algeria, Abdelhak Benchikha na Sven Vandenbroeck ambaye amewahi kuifundisha Simba kabla ya kutimkia FAR Rabat ya Morocco ambako hakudumu sana na kujiunga na Wydad Club Athletic ya nchini humo.

"Tumewapa mwezi mmoja na nusu wachezaji wetu kujitathmini, tunataka wachezaji wanaojituma ili kuendelea kusalia kikosini, nina imani kuna wachezaji watakaopoteza nafasi zao ndani ya timu," alisema Try Again na kuendelea,

"Bodi yangu na viongozi wengine hatutakuwa tayari kuona au kumvumilia mchezaji ambaye hajitumi, Simba inahitaji nyota ambao watatufikisha pale tunapotaka kufika, kutwaa mataji ya ndani na kufanya vizuri zaidi kimataifa ikiwamo kucheza nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika na hili kocha ataambiwa," alisema Try Again.

Aidha, Mkurugenzi huyo wa bodi alisema kocha wanayemtarajia kujiunga nao ni bora pia ana uzoefu mkubwa wa soka la Afrika pamoja mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Kuhusu majina yanayotajwa sifahamu ila ninachofahamu tunaleta mwalimu wa kututoa hapa kwenye robo fainali na kutupeleka nusu fainali, ni kocha mwenye uwezo mkubwa, wana Simba watulie viongozi tunafanya kazi yetu kwa umakini mkubwa," alisema.

Aidha, alisema kwa sasa wako kwenye hatua ya mwisho ya kumtambulisha kocha mpya ambaye atakuwa na jukumu kubwa la kufanya maboresho kipindi cha dirisha dogo la usajili Januari mwakani.

Katika hatua nyingine, Try Again ame-

INAENDELEA UKURASA 23

# Nzengeli, Baleke vinara ndani ya boksi

**Na Adam Fungamwango**

WAKONGOMANI wawili, kiungo mshambuliaji wa Yanga, Maxi Nzengeli na mshambuliaji wa Simba, Jean Baleke wanaongoza kwa kufunga mabao ndani ya eneo la hatari kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara hadi kufikia raundi ya tisa kabla ya kusimama kupisha kalenda ya FIFA.

Wachezaji hao wote wawili wanaongoza kwenye orodha ya wafungaji bora wakiwa na mabao saba, wamefunga mabao sita wakiwa ndani ya boksi kila mmoja.

Nzengeli aliyesajiliwa msimu huu kutokea Maniema FC ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo amepachika mabao sita akiwa ndani ya eneo la hatari na moja amelifunga akiwa nje ya eneo la hatari sawa na Baleke ambaye naye amefunga mabao sita akiwa ndani ya eneo la hatari na bao moja akifunga akiwa nje ya eneo hilo.

Hata hivyo, kwa mujibu wa dawati la takwimu la Nipashe, Nzengeli ndiye mchezaji pekee miongoni mwa wachezaji watatu wenye mabao mengi kufunga bao kwa kichwa.

Baleke na Aziz Ki ambao wote wana mabao saba kama Nzengeli lakini hawana bao walilofunga kwa kichwa.

Baleke amefunga mabao yote kwa mguu wa kulia na Aziz Ki, akifunga mabao matano kwa mguu wa kushoto na mawili mguu wa kulia.

Wakati Nzengeli na Baleke wakiwa vinara wa kupachika mabao ndani ya eneo la hatari, kiungo Mtanzania wa Azam FC, Feisal Salum anashika nafasi ya pili kwa kufunga mabao ndani ya boksi akifanya hivyo mara tatu, huku wachezaji wa Yanga, Aziz Ki na Pacome Zouzoua wakiwa kwenye nafasi ya tatu, wakipachika mabao manne wakiwa karibu na lango.

Takwimu zinaonyesha wachezaji wanaofuata ni wale ambao wamefunga mabao matatu kila mmoja ndani ya

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042